**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# WIZARA YA BIASHARA MAENDELEO YA VIWANDA

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA MAENDELEO YA VIWANDA

**MHESHIMIWA**
**OMAR SAID SHAABAN (MBM)**

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**MEI, 2022**

**YALIYOMO**


**1. UTANGULIZI ................................................... 1**

**2.MWENENDO WA BIASHARA ............................ 4**

2.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani ....................4

2.2 Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya za Kikanda (EAC na SADC).....................................................7

2.3 Hali ya Biashara Zanzibar....................................11

2.4 Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ........ (Inter- State Trade Balance) ..................................14

2.5 Hali ya Chakula na Bei Katika Soko La Zanzibar ....15

**3.HALI YA VIWANDA ........................................18**

**4.UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022..................... .22**

4.1 Ukusanyaji wa Mapato ......................................22

4.2 Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022..............................................................23

4.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara .....................23

**5. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2021-2022..................................74**

**6. PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023.................................................... 75**

**7. SHUKRANI ....................................................89**

8. **MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....................92**

8.1 Mapato ya Serikali.............................................92

8.2 Matumizi ..........................................................93

**9. HITIMISHO:.....................................................95**

**10. VIAMBATANISHO: .........................................96**

Kiambatanisho Namba 1: .............................................96
Kiambatanisho Namba 2: .............................................97
Kiambatanisho Namba 3: .............................................98
Kiambatanisho Namba 4: .............................................99
Kiambatanisho Namba 5: ...........................................100

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN, KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023:

## 1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema pamoja na kutuwezesha kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na kusherehekea sikukuu ya iddil fitri katika hali ya salama na amani. Aidha, namshukuru kwa kutuwezesha kufika katika Baraza lako hili leo ili kuendelea kutekeleza majukumu ya kujenga nchi yetu katika kipindi hiki cha awamu ya nane ya uongozi hapa Zanzibar.

2. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake imara uliojaa hekima na busara na wenye azma kubwa ya kuiletea Zanzibar maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuendelea kuongoza vyema taifa letu kwa mstakabala wa mapinduzi ya viwanda na uchumi wa buluu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa jitihada zao za dhati wanazozichukua za kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile kwa kutupatia miongozo, maelekezo na michango katika maendeleo ya nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Baraza letu la Wawakilishi. Vile vile, ninawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Baraza, kwa kufanya kazi zao kwa uadilifu, umakini na weledi. Kamati hizi zimeweza kutoa ushauri na maelekezo yanaosaidia sana utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

5. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya bajeti hii yamepitia katika hatua na ngazi mbali mbali za awali ikiwemo Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi. Naomba kuchukua fursa hii kuishukuru sana Kamati hii inayoongozwa na Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni pamoja na wajumbe wake wote kwa kuchambua mapendekezo

ya awali ya bajeti hii na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

6. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani zangu za pekee zimuendee Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Islam Seif Salum kwa msaada na mashirikiano yake makubwa anayonipatia katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Pia, nawashukuru kwa dhati Wakurugenzi na viongozi wote wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia yaliyosaidia katika utekelezaji mzuri wa majukumu yangu.

7. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya Bajeti hii yamezingatia nyenzo muhimu zifuatazo:-

   i. Maelekezo na Ahadi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein A. Mwinyi;
   ii. Malengo na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050;
   iii. Zanzibar Development Plan 2021 – 2026
   iv. Ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025
   v. Ukomo wa Rasilimali fedha uliowekwa kwa Wizara; na,
   vi. Miongozo mbalimbali ya Kisera na kisheria inayosimamiwa na Wizara.

8. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mazingatio ya hapo juu, utayarishaji wa mapendekezo haya ulizingatia pia matukio mbalimbali yaliojitokeza ulimwenguni ambayo yamekuwa na athari ya moja kwa moja katika mwenendo wa uchumi, biashara na viwanda duniani. Matukio hayo ni kama vile mwenendo wa uwekezaji duniani, maendeleo na mashirikiano ya kibiashara na Fedha, pia masuala ya kisiasa na kijamii katika baadhi ya maeneo duniani.

9. **Mheshimiwa Spika,** Katika hotuba hii, nitaanza kwa kufanya mapitio ya jumla kuhusu mwenendo wa biashara na hali ya viwanda, utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022, nitabainisha changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2021/2022 na hatimae nitawasilisha mapendekezo ya bajeti kwa programu za Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 2. MWENENDO WA BIASHARA

### 2.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani

10. **Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa uchumi wa biashara duniani umeanza kutengemaa na unaendelea kuongezeka, hali hii inapelekea ukuaji biashara Duniani kuongezeka na kupelekea mchango mkubwa katika uchumi wa dunia (World Merchandise Trade Percentage of GDP). Katika kipindi cha mwaka

2021 mchango wa biashara duniani ulifikia Dola za kimarekani trilioni 22.4 sawa na ongezeko la asilimia 9.8 la biashara iliyofanyika ukilinganisha na mwaka 2020. Kwa mwaka 2021, Biashara ilishuhudiwa kuongezeka kwa kasi baada ya kudorora kwa janga la COVID-19 mwaka 2020, lakini ukuaji ungeweza kuwa na nguvu zaidi bila ya mawimbi ya mara kwa mara ya COVID-19 katika mwaka huo.

***Usafirishaji***

**11. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya makisio ya Shirika la Biashara la Dunia (WTO) kwa kipindi cha mwaka 2021, usafirishaji wa bidhaa kwa nchi za Asia uliongezeka kwa asilimia 13.8 ukilinganisha na asilimia 0.5 kwa mwaka 2020, nchi za Ulaya umeongezeka kwa asilimia 7.9 kwa mwaka 2021 ukilinganisha na asilimia (7.8) kwa mwaka 2020. Aidha, nchi za Marekani ya Kaskazini na Marekani ya Kusini usafirishaji uliongezeka na kufikia asilimia 6.3 na 6.8 kwa mwaka 2021 ukilinganisha na asilimia (8.8) na (4.6) kwa mwaka 2020, nchi za Afrika nazo usafirishaji wake umeongezeka hadi kufikia 5.1 kwa mwaka 2021 ukilinganisha na asilimia (7.5) kwa mwaka 2020 ya usafirishaji wote duniani.

### *Uagiziaji*

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2021, uagiziaji wa bidhaa kwa nchi za Asia uliongezeka kwa asilimia 11.1 ukilinganisha na asilimia (1.0) kwa mwaka 2020, nchi za Ulaya umeongezeka kwa asilimia 8.1 kwa mwaka 2021 ukilinganisha na asilimia (7.3) kwa mwaka 2020 ya uagiziaji wote. Aidha, nchi za Marekani ya Kaskazini na Marekani ya Kusini uagiziaji uliongezeka na kufikia asilimia 12.6 na 25.8 kwa mwaka 2021 ukilinganisha na asilimia (6.1) na (11.2) kwa mwaka 2020, nchi za Afrika nazo uagiziaji wake umeongezeka hadi kufikia 4.2 kwa mwaka 2021 ukilinganisha na (11.8) ya uagiziaji wote duniani.

13. **Mheshimiwa Spika,** Kuongezeka kwa kiwango cha biashara kimetokana na kupunguwa kwa mawimbi ya UVIKO - 19 kwa nchi zilizoendelea ikiwemo bara la Ulaya na Marekani kwa mwaka 2021. Hata hivyo, kwa mwaka 2022, takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha biashara za bidhaa duniani kinategemewa kupungua kwa asilimia 3.0, lakini takwimu hizi zinaweza kubadilika kutokana na kutokuwa na uhakika kuhusu mwenendo wa mgogoro wa Ukraine.


## 2.2 Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya za Kikanda (EAC na SADC)

### JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)

***Usafirishaji***

14. **Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inajumuisha nchi Saba (7) ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Congo DRC iliyojiunga hivi karibuni. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina ubia wa biashara ya kuagiza na kuuza kutoka nchi hizi.

15. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imefanya biashara ya kusafirisha duniani kote bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 155.672** kwa mwaka 2021 kati ya hizo **Shilingi bilioni 3.574** ambayo ni sawa na asilimia **2.3** ya usafirishaji wote ulifanyika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ikilinganishwa na biashara ya **shilingi milioni 628.1** mwaka 2020. Usafirishaji huo ulifanyika zaidi katika nchi ya Kenya kwa bidhaa za Kanga na Vitenge kama inavyoonekana katika **Mchoro namba 1** hapa chini.





***Chanzo: WBMV kutokana na Takwimu za OCGS, 2021***

### *Uagiziaji*

**16. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji kwa mwaka 2021 Zanzibar imeagiza duniani kote bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 968.6, kati ya hizo, bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 7.2 ambayo ni sawa na asilimia 0.7 ya uagiziaji wote zimetoka katika nchi za EAC, ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.4 sawa na asilimia 0.6 ya uagiziaji kwa mwaka 2020. Kiwango kikubwa cha uagiziaji kimetoka nchi ya Kenya ambapo bidhaa ya Saruji imeongoza kwenye uagiziaji huo. **Mchoro namba 2** hapa chini unaonesha uagiziaji kwa nchi za EAC.

## Mchoro Namba 2: Uagiziaji wa Bidhaa kwa Nchi za EAC kwa mwaka 2021




***Chanzo: WBMV kutokana na Takwimu za OCGS, 2021***


## JUMUIYA YA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)

### *Usafirishaji*

**17. Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) inajumuisha nchi wanachama 16 ikiwemo Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ambapo Zanzibar ni miongoni mwa nchi hiyo. Kwa mwaka 2021/2022 Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 2.406 ambayo ni sawa na asilimia 1.5 ya usafirishaji wote kwa nchi za SADC ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo bidhaa zenye thamani ya shilingi milioni 799.2 zilisafirishwa zikiwemo nguo na bidhaa za vyakula kama vile dagaa. Katika usafirishaji huo nchi ya Afrika Kusini iliongoza kuagiza bidhaa kutoka

Zanzibar zenye thamani ya shilingi bilioni 1.228 kama inavyo onekana katika **Mchoro Namba 3** hapo chini;

**Mchoro Namba 3: Usafirishaji wa Bidhaa kwa Nchi za SADC kwa mwaka 2021**





***Chanzo: WBMV kutokana na Takwimu za OCGS, 2021***

***Uagiziaji***

**18. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Zanzibar imeagiza bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 7.823 kutoka nchi za SADC, ambayo ni sawa na asilimia 0.8 ya uagiziaji wote. Uagiziaji wa bidhaa kwa nchi za SADC kwa mwaka 2021 umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo jumla ya bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 6.15 ziliagizwa. Afrika ya Kusini imeongoza kwa kuingiza bidhaa Zanzibar zenye thamani ya shilingi bilioni 6.88

kwa mwaka 2021 kwa bidhaa za nguzo za mbao na mita za malipo. **Mchoro Nambari 4** hapo chini unaonesha thamani ya uagiziaji kwa nchi za SADC kuja Zanzibar.

**Mchoro Namba 4: Uagiziaji wa Bidhaa kwa Nchi za SADC kwa mwaka 2021**




***Chanzo: WBMV kutokana na Takwimu za OCGS, 2021***

## 2.3 Hali ya Biashara Zanzibar

***Usafirishaji***

**19. Mheshimiwa Spika,** Hali ya biashara kwa ujumla imeendelea kuimarika kwa kipindi cha mwaka 2021, ambapo Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya **shilingi trilioni 1.12** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 913.09** kwa mwaka 2020 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 23.1.** Biashara hiyo ilikuwa

ni usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Zanzibar na uagiziaji wa bidhaa kuingia Zanzibar.

20. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Zanzibar imesafirisha nje bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 155.62.** Kiwango hicho cha usafirishaji ni sawa na ongezeko la **asilimia 137** ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 65.66 uliofanyika kipindi cha mwaka 2020. Bidhaa zilizosafirishwa nchi za nje ni pamoja na karafuu, mwani na mazao ya baharini. Katika usafirishaji huo, zao la karafuu lilikuwa na thamani ya **shilingi bilioni 115.36** sawa na **asilimia 74.1** ya usafirishaji wote. Ongezeko hilo limechangiwa na kupanda kwa bei ya karafuu na msimu mkubwa wa uzalishaji. Miongoni mwa nchi zilizonunua karafuu ni pamoja na Singapore, India, Denmark na nchi za Falme za Kiarabu (UAE).


***Uagiziaji***

21. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Zanzibar imeagiza bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 968.64 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 847.43 kwa mwaka 2020. Bidhaa ambazo Zanzibar imeagiza kutoka nchi za nje ni pamoja na vyombo vya usafiri, bidhaa za Kielektroniki (Kompyuta, Simu),

Mashine, bidhaa za Nguo na bidhaa za Chakula. Nchi ambazo tumeagiza bidhaa kwa wingi ni pamoja na nchi za Falme za Kiarabu, China na India.

**22. Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa biashara umeonesha kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara kutoka **shilingi bilioni 781.76** kwa mwaka 2020 hadi **shilingi bilioni 812.97** kwa mwaka 2021. Ongezeko hilo linaonesha kutofanya vizuri uzalishaji wa ndani ya nchi na kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa nchini ikiwemo bidhaa za Chakula, Vifaa vya Usafiri, Mashine ambavyo vina thamani kubwa. **Mchoro namba 5** hapo chini unaonesha hali hii.

**Mchoro Namba 5**
**Mwenendo wa biashara Zanzibar (2017-2021).**




***Chanzo: limechorwa na WBVM kutokana na Takwimu za OCGS, 2021***

## 2.4 Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Inter- State Trade Balance)

**23. Mheshimiwa Spika,** Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha utoaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania bara na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Biashara hiyo inahusisha bidhaa za vyakula vikiwemo Mchele, Mbatata, Maharage, Vitunguu, Tungule na Mboga, Viazi vitamu, Matunda; vitu vya Kielektroniki; vifaa vya usafiri ikiwemo Gari, pikipiki pamoja na Dawa na Vinywaji.

***Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa***

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2021, Zanzibar imesafirisha bidhaa kwenda Tanzania Bara zenye thamani ya **shilingi bilioni 33.99** ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 15.03** zilizosafirishwa mwaka 2020. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta ya kupikia Tanzania bara, chuma chakavu, dagaa, vitenge, pamoja na vitu mchanganyiko kama vile biscuit, chocolate, pipi, busati, vitambaa, kapeti na vitu vya mitumba (Used Goods).

**25. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji katika kipindi cha mwaka 2021, Zanzibar imeagizia

bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 288.26** kutoka Tanzania Bara ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 243.81** kwa mwaka 2020. Uingizaji mkubwa kutoka Tanzania bara umetokana na bidhaa za Kilimo, Chakula, Gari, Vinywaji na Dawa.

## 2.5 Hali ya Chakula na Bei Katika Soko La Zanzibar

26. **Mheshimiwa Spika**, Hali ya uwepo wa bidhaa muhimu za chakula hapa Zanzibar kwa mwaka 2021/2022 umeendelea kuridhisha na vyakula vyote vimeendelea kupatikana bila ya usumbufu wowote. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, jumla ya Tani 47,228 za Mchele, Tani 35,342 za Sukari, Tani 7,041 za Unga wa Ngano na tani 99,450 za Mafuta ya kupikia zimeingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani. Bidhaa zilizoingizwa zimetoka nchi mbali mbali ikiwemo India, Brazil, Uturuki, Pakistani, Australia, Urusi, Agentina na Vietnam.

27. **Mheshimiwa Spika,** Hata, hivyo uzalishaji wa ndani umeendelea kama kawaida kwa bidhaa ya Unga wa Ngano na Sukari. Takwimu zinaonesha jumla ya tani 42,461 za Unga wa Ngano zimezalishwa nchini kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 na kufikia tani 49,502 za Unga wa Ngano. Jumla ya tani 4,000 za Sukari zimezalishwa nchini kwa kipindi cha Julai

2021 hadi Machi 2022 na kiwanda cha Zanzibar Sugar Factory Limited kilichopo Mahonda na kufikia tani 39,342 za Sukari zilizokuwepo nchini. Kwa upande wa makisio ya matumizi ya bidhaa hizo, Zanzibar inatumia wastani wa tani 10,169 za Mchele, tani 3,000 za Sukari, tani 3,679 za Unga wa Ngano na tani 418 za Mafuta ya kupikia kwa mwezi. **Jadweli nambari 1** inaonesha taarifa hizo.

**Jadweli Namba 1:**
**Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu katika Soko la Zanzibar (Julai 2021-Machi, 2022) (Tani)**

| | Bidhaa/Tani | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Mchele** | **Sukari** | **Unga wa ngano** | **Mafuta ya kula** |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka nje ya nchi | 43,667 | 35,342 | 4,000 | 99,450 |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka T. Bara | 3,621 | - | 3,041 | - |
| Bidhaa Zilizozalishwa nchini | - | 4,000 | 42,461 | - |
| **Jumla ya Bidhaa** | **47,228** | **39,342** | **49,502** | **136,072** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2022***

**28. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa bei za bidhaa muhimu kama vile Mchele, Unga wa Ngano pamoja na Sukari katika soko la ndani zimekuwa zikiongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hizo katika masoko ya dunia pamoja na gharama za usafirishaji. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali kwa kushirikiana na wafanyabiashara iliendelea na utaratibu wa kupanga bei elekezi na kusimamia bei hizo kwa lengo la kuleta unafuu wa bei kwa wananchi wa Zanzibar.

**Jadweli Namba2:**

**Wastani wa Beiza Reja Reja (Kg) za Chakula Muhimu Katika Soko la Zanzibar, 2021/2022**

| Mwezi | Mchele wa Basmati /kg | Mchele aina nyengine / kg | Mchele wa Mbeya/kg | Unga wa ngano /kg | Sukari /kg |
|---|---|---|---|---|---|
| **Julai** | 3,500 | 1,600 | 1,500-2,400 | 1,500 | 1,800-1,900 |
| **Augosti** | 3,600 | 1,600 | 1,500-2,400 | 1,600 | 1,900 |
| **Septemba** | 3,600 | 1,600 | 1,500-2,400 | 1,600 | 2,000 |
| **Oktoba** | 3,500 | 1,600 | 1,500-2,400 | 1,600 | 2,000 |
| **Novemba** | 3,600 | 1,600 | 1,600-2,600 | 1,600 | 2,000 |
| **Disemba** | 3,500 | 1,600 | 1,800-2,800 | 1,600-1800 | 2,000 |
| **Januari** | 3,500 | 1,600 -1,700 | 1,800-3,000 | 1,600-1,800 | 2,000 |
| **Februari** | 3,600 | 1,600-1,700 | 1,800-3,000 | 1,700-1,800 | 2,000-2,200 |
| **Machi** | 3,500 - 4,000 | 1,600 -1,700 | 1,800-3,000 | 1,700-1,800 | 2,000-2,200 |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2022***


# 3. HALI YA VIWANDA

29. **Mheshimiwa Spika,** Mchango wa Viwanda katika pato la Taifa umeendelea kuimarika kutoka **asilimia 18.3** mwaka 2020 hadi kufikia **asilimia 19.6** mwaka 2021 hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 1.5** ambapo sekta ya uzalishaji Viwandani ilichangia asilimia 7.7 kutoka **asilimia 6.6** mwaka 2020. Hali hiyo inakwenda sambamba na utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 – 2025 ambayo imeelekeza mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa kuongezeka

hadi **asilimia 22.5** ifikapo mwaka 2025. **Mchoro Nambari 6** unaonesha muhtasari mchango wa kisekta katika pato la taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021

**Mchoro Namba 6**


**Mchango wa Kisekta katika Pato la Taifa, 2020/21**




**Chanzo:** *Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali*

**30.** **Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa ukuaji wa sekta ya viwanda umeendelea kuimarika kwa kipindi cha muongo mmoja (2011 – 2020). Hali hiyo imetokana na kukua kwa sekta ya ujenzi pamoja na kuimarika kwa sekta ndogo ya uzalishaji kiviwanda ambapo viwanda vikubwa na vya kati vinaendelea kujengwa Pemba na Unguja. **Mchoro nambari 7** unaonesha mwenendo wa ukuaji wa sekta ya viwanda kwa mwaka 2011 hadi 2020.

## Mchoro Namba 7
## Ukuaji wa Sekta ya Viwanda 2011 - 2020




***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***

### 3.1 Hali ya Uzalishaji Katika Viwanda Vikubwa Nchini

**31. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara imeendelea kufanya juhudi mbali mbali kuhakikisha kwamba sekta ya viwanda inaimarika na mchango wake unaongezeka siku hadi siku. Kiujumla, hali ya uzalishaji bidhaa viwandani kwa mwaka 2021/2022 inaendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa changamoto ya ushindani wa soko kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani hapa Zanzibar na zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

**32. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation (ZMCL) kilichopo Mtoni kinachozalisha bidhaa ya unga wa ngano kimeongezewa uwezo (installation of new storage facilities and new mills)

na kimekuwa na uwezo wa kuzalisha tani 119,880 za unga wa ngano badala ya tani 64,800 kwa mwaka kwa wafanyakazi 137. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya tani 29,654.1 za unga wa ngano sawa na **asilimia 45.76** ya uwezo wa kiwanda, tani 9,660.63 za pumba (bran) na tani 1,175.58 za pollard zimezalishwa.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha maziwa cha ADPL kilichopo Fumba chenye uwezo wa kuzalisha lita 64,800,000 kwa mwaka ambacho kimeajiri wafanyakazi 67, kimeweza kuzalisha lita 1,155,095 za maziwa hadi kufikia Disemba 2021 sawa na asilimia 1.78 ya uwezo wake (installed capacity). Hata hivyo, Kiwanda hicho kimefungwa mapema mwezi Februari, 2022 kutokana na changamoto za kiushindani katika soko kwa nyakati tofauti. Wizara inaendelea na majadiliano na mwekezaji ili kutafuta suluhisho la kukifungua tena kiwanda hicho.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha AMOS Industries kilichopo eneo la viwanda la Chamanangwe ndio kiwanda cha kwanza cha kuzalisha maji ya kunywa kwa upande wa Pemba. Ujenzi wa kiwanda hicho umekamilika na kazi ya kufunga mitambo inaendelea. Kiwanda kinatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 1.8 na kutoa ajira 50 za moja kwa moja kiwandani hapo na

ajira 60 nje ya kiwanda. Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita elfu tano (5,000 lita) za maji kwa saa moja. Maji ya kiwanda hicho yatajulikana kwa jina la kibiashara “lulu”. Katika hatua nyengine kampuni hiyo ina mpango wa kuongeza laini (Mashine) ya kuzalisha juisi ya matunda ambapo kiwanda kitasaidia sana kupunguza upotevu wa matunda (post harvest loss) yanayolimwa Pemba.

35. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha nguo cha Basra Textile Mills Limited Kilichopo Chumbuni ambacho kimezinduliwa rasmi mnamo tarehe 11 Januari 2022, kimeanza uzalishaji wa bidhaa za vitenge tangu Disemba 2020, ambapo jumla ya wafanyakazi 314 wameajiriwa kwenye kiwanda hicho. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kiwanda kimeweza kuzalisha takriban mita 14,500,741 za vitenge na kuingia katika masoko ya nchi za Afrika Mashariki na SADC.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2021 / 2022 jumla ya viwanda 10 vimezinduliwa na kuwekewa jiwe la msingi. Viwanda hivi ni vya kati (medium sized industries) na vinatarajia kutoa wastani wa ajira 400 katika mwendelezo wa kuzalisha ajira 300,000 zilizoahidiwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 - 2025. Kiambatanisho Namba 1 kinaonesha viwanda hivyo.

## 4. UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022

### 4.1 Ukusanyaji wa Mapato

**37. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kukusanya mapato ya **shilingi bilioni 2.84** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali. Hadi kufikia 31 Machi, 2022 jumla ya **Shilingi bilioni 2.15** zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na **asilimia 76** ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Vile vile, Wizara imekusanya ushuru wa stampu na mapato mengineyo yenye thamani ya jumla ya **shilingi milioni 603.04** na kufanya makusanyo yote kuwa **shilingi bilioni 2.75** ambapo ni sawa na **asilimia 97** ya makusanyo kwa mwaka husika. Mchanganuo wa mapato unapatikana katika kiambatanisho **namba 2. Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla taasisi na idara zote zimefanya vizuri katika ukusanyaji mapato, kwa ongezeko la mapato katika baadhi ya vifungu umetokana na kuanza kufunguka kwa shughuli za kibiashara, usajili wa vyombo vya moto na upimaji wa mafuta yanayoingia nchini.

## 4.2 Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya **Shilingi bilioni 30.54** kwa ajili ya kutekeleza programu zake. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Julai – Machi, 2021/2022, Wizara ilipanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 25.99 Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022, jumla ya **Shilingi bilioni 5.31** sawa na **asilimia 20.4** ya matumizi kwa kipindi cha miezi tisa ambazo ni sawa na **asilimia 17** ya makisio ya mwaka, ziliingizwa kwa ajili ya matumizi hayo. Kati ya hizo **Shilingi bilioni 3.23** kwa ajili ya malipo ya mishahara, **Shilingi bilioni 1.37** kwa kazi za kawaida na **Shilingi milioni 707.68** kwa kazi za maendeleo. Mchanganuo wa matumizi hayo kwa kila program ulikuwa kama unavyoonekana katika **Kiambatanisho Namba 3.**

## 4.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara

39. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ulifanyika kulingana na huduma na shughuli zilizowekwa katika programu kuu Tatu za Wizara kama ifuatavyo:

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imeundwa na Programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji wa Wizara; Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti; na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Katika kutekeleza majukumu yake, program hii ilipangiwa matumizi ya **Shilingi bilioni 3.03** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, hadi kufikia Machi 2022, programu hii imeingiziwa jumla ya **Shilingi bilioni 1.82** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na **asilimia 60** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

### Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara:

41. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni pamoja na huduma ya ununuzi wa vifaa vya ofisi na usafiri, huduma ya usimamizi wa rasilimali watu na

huduma kwa ujumla pamoja na kuratibu mikutano ya majadiliano ya kibiashara na viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya Shilingi bilioni 1.86 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya Shilingi bilioni 1.14 ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia 61 ya makadirio ya mwaka. Huduma za Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji zilitekelezwa kama ifuatavyo:-

***Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma kwa Ujumla***

42. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuongeza uwajibikaji, Wizara imeendelea kutekeleza mpango wake wa mafunzo ambapo jumla ya wafanyakazi watatu (3) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, kati ya hao wawili (2) ngazi ya shahada ya pili ya Uongozi wa biashara, Uhandisi wa Viwanda na mmoja (1) shahada ya kwanza ya Utunzaji Kumbukumbu. Pia, wafanyakazi nane (8) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya udereva, utunzaji nyaraka na kumbukumbu.

43. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imezingatia pia masuala ya mahitaji ya mafunzo katika masuala mtambuka kwa wafanyakazi wake. Kwa kuzingatia hilo, wafanyakazi

wamepatiwa mafunzo ya kuzuia rushwa katika maeneo ya kazi, kupambana na uhujumu uchumi pamoja na njia bora ya kuzuia kuenea kwa maradhi. Aidha, wafanyakazi walipatiwa uelewa wa Sheria namba 2 ya utumishi wa umma ya mwaka 2011 yenye lengo la kuwatanabahisha kuhusu haki, wajibu, makosa na adhabu zilizomo ndani ya sheria hiyo. Vile vile, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya kiutendaji (Performance Appraisal) kwa wafanyakazi wake na kutoa nyongeza ya mshahara kwa wenye kustahiki kwa kuzingatia muongozo wa utumishi wa umma serikalini.

44. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha haki na maslahi ya wafanyakazi yanazingatiwa, Wizara imewapatia wafanyakazi 61 likizo zao za kimsingi, kati ya hao wafanyakazi 41 likizo la kawaida, wafanyakazi 16 likizo la dharura na wafanyakazi 4 likizo la uzazi. Aidha, wafanyakazi 7 wamepatiwa huduma ya mazishi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na wafanyakazi 6 wamestaafu kazi kwa kutimia umri wa lazima.

45. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imefanya ukarabati mdogo katika ofisi zake kwa kutengeneza sehemu za vyoo, mifumo ya maji taka na maji safi pamoja na mfumo wa nishati ya umeme. Aidha, Wizara imeliorodhesha jengo lake

la Bizanje katika mnada wa Mamlaka ya mji Mkongwe kama maagizo ya serikali yalivyoelekeza. Lengo ni kuweza kujenga jengo la ofisi jipya na la muonekano wa kisasa kupitia fedha zitakazopatikana katika uuzaji wa jengo hilo.

***Huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi***

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia mpango wa manunuzi wa Wizara kwa kufuata taratibu za kizabuni. Manunuzi yaliofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni pamoja na vifaa vya kuandikia, matengenezo ya magari, ununuzi wa mafuta na upambaji kwa ajili ya sherehe za kitaifa. Vile vile, Wizara imedhibiti mapato na matumizi ya fedha kwa kufuata kikamilifu miongozo, kanuni na taratibu za serikali ambapo taarifa ya utekelezaji wa mapato na matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka na mwaka imeandaliwa.

***Uratibu wa Mikutano ya Majadiliano ya Kibiashara na Viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa***

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha ushiriki wa viongozi wa Wizara katika mikutano ya kisekta ya Biashara na Viwanda ya Ndani, Kikanda na Kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara

imeratibu na kushiriki mikutano 10 ya Kikanda, Kitaifa na Kimataifa ikiwemo ushiriki wa maonesho ya Kimataifa ya EXPO Dubai 2020. Aidha, Kongamano la tatu la uchumi wa biashara kati ya Uturuki na Afrika, Mkutano wa dharura wa Baraza la Mawaziri na Kamati ya fedha, uchumi na biashara imehudhuriwa.

## Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

48. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii ndogo imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutayarisha, kuchambua na kutathmini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya Wizara. Huduma ambazo zimesimamiwa na Programu hii ndogo ni Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara, Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara na Usimamizi wa Takwimu za Biashara na Viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya Shilingi milioni 576.13 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya Shilingi milioni 223.91 ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia 39 ya makadirio ya mwaka.

### *Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara*

49. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha mipango ya Wizara inatekelezwa kwa kuzingatia sera na mikakati iliopo, Wizara imeandaa rasimu ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sera ya Maendeleo ya sekta binafsi ya mwaka 2020. Rasimu hiyo imeonesha taratibu na mfumo utakaotumika katika kufanya ufuatiliaji wa mikakati iliomo ndani ya sera hiyo. Aidha, kikao cha kutoa uwelewa kwa wadau juu ya Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi kimefanyika kwa taasisi za serikali na binafsi.

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha utafiti wa sheria ya Leseni za Biashara namba 3 ya mwaka 1983 kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria, Zanzibar. Matokeo ya utafiti huo imeonesha kutokutekelezeka kwa vifungu vingi vilivyomo ndani ya sheria hiyo na kutokuainisha wazi utaratibu mzuri wa usimamizi wa leseni za biashara kupitia Mamlaka mbali mbali zinazotoa leseni Zanzibar. Imependekezwa kuandaliwe sheria mpya itakayoweka mfumo mzuri zaidi wa biashara na kuunganisha biashara mbalimbali zinazohusiana na kumilikiwa na mtu mmoja. Aidha, Mpango wa Utafiti wa Wizara (Research Master Plan) kwa kipindi cha miaka mitano umekamilika ambao umependekeza maeneo ya kufanya tafiti mbalimbali za Biashara na viwanda.

### *Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara*

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa mazingira mazuri ya ufanyaji biashara na viwanda ili kuweza kuyafikia malengo tuliojipangia. Kwa kuhakikisha hilo, Wizara imefanya mapitio ya Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Wizara unaotumia muongozo mpya wa "Score Card" ambao unakwenda sambamba na dira ya Serikali ya Uchumi wa Bluu. Pia, Wizara imechapisha vitabu 50 vya Mkakati wa Mawasiliano na kusambazwa kwa taasisi na Idara kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wake.

52. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha utekelezaji unafikiwa kwa ufanisi zaidi, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo kwa kazi za maendeleo kwa Taasisi na Idara zinazosimamia miradi ya maendeleo. Taarifa ya ufuatiliaji imeandaliwa na kuwasilishwa Tume ya Mipango kwa hatua zaidi. Aidha, ripoti za utekelezaji kwa kipindi cha robo mwaka zimeandaliwa pamoja na kuandaa vipaumbele vya sekta ya biashara na viwanda kwa mwaka wa fedha 2022/2023.**Vile vile,** Mafunzo ya Bajeti kwa kuzingatia mfumo mpya wa Uandaaji bajeti (Zanzibar Planning, Budgeting and Reporting System – ZanPBRS) yamefanyika kwa maafisa wa idara na taasisi za Wizara.

### *Usimamizi wa Takwimu za Biashara*

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeweza kutatua changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika uchambuzi wa takwimu za biashara na viwanda kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Wizara 27 yanayohusiana na uchambuzi wa taarifa kwa kutumia "EXCEL". Aidha taarifa za takwimu za Biashara na Viwanda kwa robo mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa hatua zinazofuata. Vile vile, Wizara imeimarisha Ofisi ya takwimu iliopo bandarini kwa kufanya ununuzi wa vifaa muhimu vya kufanyia kazi.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha utafiti mdogo "Survey" ya "Convention factor" iliyohusiana na vipimo rasmi vya kupimia mizigo ya biashara bandarini kama vile Kilogram, Tani au lita, badala yake kumekuwa na utumiaji wa vipimo visivyo rasmi kama Polo, Roba, Gunia, Box, ambavyo hupelekea kukosa vipimo vilivyo rasmi vinavyotumika kitaifa na kimataifa. Matokeo ya utafiti huo mdogo yamewezesha kupata uzito wa wastani kwa mizigo inayoingizwa kutoka Tanzania bara kama ifuatavyo: mchele ambao hurikodiwa kwa polo, uzito wake ni baina ya kilo 50-75 (wastani wa kilo 62), Vitunguu maji ambavyo hurikodiwa kwa gunia, uzito wake ni baina ya kilo 120-125 (wastani wa kilo 125), na polo za Mbatata kwa kawaida uzito wake ni baina ya kilo 102-113 wastani wa kilo 107.

## Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

55. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kutekeleza na kusimamia shughuli zote za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa upande wa Pemba. Huduma ambayo inasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **Shilingi milioni 602.86** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na hadi kufikia 31 Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 457.30** ikiwa ni mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na **asilimia 76** ya makadirio ya mwaka. Huduma iliyopangwa kutolewa na Programu hii imetekelezwa kama ifuatavyo:-

***Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba***

56. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua ya kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali Wizara imetembelea jumla ya vikundi 72 vya wajasiriamali na kuandaa mikutano mitano (5) kwa lengo la kusikiliza changamoto zao na kuweza kuzitatua kwa pamoja katika Wilaya zote za Pemba. Kati ya vikundi hivyo, vikundi Sitini (60) vimepatiwa mafunzo ya utengenezaji (usarifu)

wa bidhaa kwa kutumia mwani ili kuhakikisha mwani tunautumia kwa matumizi ya ndani mbali ya kusafirisha. Bidhaa ambazo zilizozalishwa ni Sabuni, losheni, mafuta ya nywele, mafuta ya kujipaka, Juisi pamoja na Jamu. Aidha, vikundi kumi na tisa (19) kati ya hivyo vilipata nafasi ya kushiriki katika maonesho ya saba saba Tanzania Bara na kushiriki Tamasha la nane (8) la Biashara la Zanzibar.

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara kupitia Ofisi kuu Pemba imefanya Vikao vitatu (3) na wafanyabiashara juu ya kuthibiti ongezeko la bei za bidhaa muhimu kwa lengo la kuhakikisha wafanyabiashara hawaendi kinyume na bei elekezi iliowekwa na serikali kwa bidhaa ya Mchele, Sukari, Unga wa Ngano na Mafuta ya kupikia. Sambamba na hilo, Wizara imefanya mapitio katika maduka ya Wilaya nne za Pemba ili kujiridhisha kuwa bei elekezi iliyotangazwa na Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inafuatwa na wafanyabiashara wote wa Pemba.

58. **Mheshimiwa Spika,** Wizara Biashara Pemba imeratibu ujenzi wa sehemu ya kukaushia Mwani kwa kutumia jua katika Wilaya ya Micheweni kwa wakulima wa mwani Makangale. Kaushio ambalo lilijengwa kwa Ufadhili wa TIRDO ili kupunguza changamoto ya kuoza kwa mwani kipindi cha mvua.

59. **Mheshimiwa Spika,** Pia, Wizara ilisimamia na kuratibu shughuli za uanzishwaji wa Viwanda, ambapo Viwanda viwili vikubwa vya uzalishaji maji safi ya kunywa vimejengwa katika Wilaya ya Wete kimoja ni AMOS katika eneo la Chamanangwe, na cha pili ni Water Com katika kijiji cha Kinyikani Wete Pemba.

60. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua ya kumlinda mtumiaji, Wizara imefanya ukaguzi wa mizani 549, mita ndogo za mafuta 39, mita kubwa 3 za kutolea mafuta katika bandari ya Wesha, magari 8 ya kubebea mafuta na matangi 6 ya mafuta ya chini yamekaguliwa katika shehia mbali mbali za wilaya zote za Pemba. Pia, Wizara imefanya ukaguzi wa Maduka 1,135, Bekari 66 na Maghala 106.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda ambayo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA) inajumuisha Programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Program hii kuu ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 13.72** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii kuu imeingiziwa jumla ya

**Shilingi milioni 579.24** ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida, sawa na **asilimia 4.2** ya fedha zilizopangwa kwa mwaka. Program ndogo hizo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

## Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji wa Viwanda inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kutoa huduma ya kuimarisha sekta ya viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 3.36** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 426.09** ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengineza kawaida, sawa na **asilimia 13** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa program ndogo ya Ukuzaji Viwanda ulikuwa kama ifuatavyo:-

### *Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda*

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda katika kuendeleza maeneo ya Viwanda nchini, imefanya tathmini kwa eneo la Nungwi ambapo ripoti imeonesha jumla ya shilingi milioni 801 zinahitajika kwaajili ya fidia. Aidha mchakato wa kumtafuta mshauri elekezi wa kuandaa Mpango

Mkuu (detailed master plan) na upembuzi yakinifu (feasibility study) zimeanza ambapo tangazo la zabuni limetolewa. Sambamba na hayo, upimaji wa eneo la Dunga umekamilika na taratibu za kufanya tathmini ya fidia katika eneo hilo zimeanza. Vilevile zoezi la ujenzi wa barabara rafiki ya kuingilia katika eneo la Dunga zimeanza kwa kufanya survey ya eneo kwa mashirikiano na wataalamu kutoka idara ya barabara kwa kuweka mipaka eneo hilo la viwanda.

64. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuratibu shughuli za uanzishaji wa kiwanda cha mwani Pemba, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda imefanya kikao na Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi katika eneo la Chamanangwe. Kikao hicho kilijadili juu ya namna ya kuliendeleza eneo la Chamanangwe kiujumla wake, ikiwemo njia bora za kutumia katika kuhakikisha wananchi wote wanachukua pesa zao kwa maridhiano baina ya Serikali na wananchi hao. Aidha kikao pia kilijadili juu ya ujenzi wa Kiwanda cha Mwani na kushauri Wizara kuharakisha mchakato wa ujenzi wa kiwanda hicho.

65. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua za kutekeleza mradi wa kuendeleza maeneo ya viwanda, Wizara ilifanya mazungumzo na Uongozi wa Benki ya Afrexim uliyoongozwa na Makamu wa Raisi wa benki hiyo juu ya uwezekano wa kuyafanyia upembuzi yakinifu

na kuandaa Mpango Mkuu wa matumizi wa maeneo ya Viwanda ya Dunga na Chamanangwe. Baada ya Mazungumzo hayo, mnamo tarehe 18/02/2022 Wizara ilitia saini mashirikiano ya awali (MOU) na Afrexim Bank kwaajili ya kuandaa nyaraka (Bankable Feasibility study and Detailed Master plan). Majadiliano yanaendelea kuhusiana na utekelezaji wa mashirikiano haya.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo (SMZ) kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (SMT) imetayarisha Mpango wa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na UNIDO kwa kipindi cha miaka mitano ijayo 2021 – 2025. Katika Mpango huu (PCP), Tanzania inatarajia kufaidika kwa kuendeleza miradi mikubwa ya viwanda, kuendeleza mnyororo wa thamani kwa mazao ya kilimo na kuhakikisha Tanzania inapata teknolojia mpya katika masuala ya uzalishaji kiviwanda.

67. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda kwa ushirikiano na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara SMT imeanzisha dawati la KAIZEN kwa ufadhili wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan - JICA kwa lengo la kuendeleza kutoa elimu ya kuongeza ufanisi katika uzalishaji kiviwanda ili kuongeza tija na ushindani katika soko la bidhaa.

### Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA) kupitia huduma ya uratibu na utekelezaji wa sera ya MSME's na ukuzaji wa MSME's na uendelezaji ujasiriamali. Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ina jukumu la kuongeza mchango wa uzalishaji wa sekta ya ujasiriamali katika pato la Taifa. Program hii ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 10.36** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 153.16** ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida, sawa na **asilimia 1.5** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma hizo ulikuwa kama ifuatavyo:-

***Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's***

69. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda yenye lengo la kuratibu na kutekeleza sera ya MSME's. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 idara, kupitia huduma hii ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 81.0** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 13.2** sawa na **asilimia 16** ya makadirio ya mwaka.

70. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wajasiriamali wa Zanzibar wanamudu ushindani wa masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda imefanya mkutano na wajasiriamali wa usarifu wa bidhaa za mwani na wakulima wa mwani, ambapo jumla ya wasarifu 75 na wakulima 66 walipatiwa mafunzo ya masoko, branding, uwekaji kumbukumbu na usimamizi wa biashara.

71. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imetoa mafunzo kwa wakufunzi kumi (10) wa Dagaa kwa upande wa Unguja na kumi (10) wa mwani kwa upande wa Pemba. Mafunzo hayo yalijumuisha Wajasiriamali wenyewe pamoja na maafisa kutoka LGAs wanaohusika na usimamizi wa Mwani na Dagaa. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wajasiriamali na watendaji wa serikali kwa kuzingatia mnyororo mzima wa mazao hayo. Pia jumla ya washiriki 30 wamepatiwa mafunzo kutoka katika taasisi za serikali na sekta binafsi zinazohusika lengo ni kuweza kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

72. **Vile vile,** Wizara imefanya utafiti mdogo wa kuangalia mahitaji ya wajasiriamali na taasisis zinazosimamia sekta ya mwani na dagaa. Miongoni mwa matokeo ya utafiti huo ni pamoja na uwepo wa miundombinu hafifu kwa sekta hizo na ukosefu wa maeneo ya

pamoja kusarifu mazao hayo. Aidha, utafiti huo umetoa mapendekezo ya namna bora ya kuweza kuiendeleza na kuikuza sekta hiyo.

**Ukuzaji wa MSME's na Uendelezaji wa Ujasiriamali**

73. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA) yenye lengo la kuwakuza na kuwaendeleza Wajasiriamali. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 SMIDA kupitia huduma hii ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 10.3 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ikiwemo KHALIFA FUND, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 SMIDA imeingiziwa jumla ya Shilingi milioni 140.0 sawa na asilimia 1.4 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Fedha kwa ajili ya Mfuko wa kuwaendeleza wajasiriamali (Khalifa Fund) shilingi bilioni 4.37 zimeingizwa mwezi Machi,2022 bado hazijatumika, utaratibu unaandaliwa ili ziweze kuleta tija iliyokusudiwa.

74. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia SMIDA imeandaa Mashindano ya Ubunifu ngazi ya Mkoa, na Taifa pamoja na kuwaendeleza Washindi wa Ubunifu, ambapo mashindano 2 ya ubunifu yamefanyika. Washindi 5 katika ngazi ya Mkoa wamepatiwa zawadi za pesa taslim na watashindanishwa katika mashindano ya ubunifu Ngazi ya Taifa. Jumla ya wabunifu 12 walishiriki na kukabidhiwa vyeti. Mashindano hayo yalishindanishwa kwa kada ya IT, Utalii, Uvuvi, Bandari, Mwani, Mafuta

na Gesi.

75. **Mheshimiwa Spika,** SMIDA imehamasisha uingizaji wa Teknolojia mpya na kushajihisha matumizi yake, hivyo watendaji 2 wa SMIDA na Wanafunzi 3 kutoka KIST wanaendelea na mafunzo ya utengenezaji wa mashine ya kusagia mwani, Teknolojia hiyo mpya imetokana na ubunifu wa Ndg. Ria Wanimo Dosa, Watendaji wa SMIDA na KIST wameweza kuisoma mashine hiyo na kuandaa michoro na wanaendelea na utengenezaji wa mashine na kwa sasa zoezi hilo limefikia asilimia 62.

76. **Mheshimiwa Spika,** SMIDA inaendelea na uendeshaji wa Kituo cha Mafunzo ya kusarifu mazao ya kilimo Kizimbani kwa Unguja na Pemba, huduma ya umeme, pamoja na kuwapatia nafasi baadhi ya wajasiriamali wazalishaji (Vijana) waliopatiwa mafunzo kuweza kutumia kituo hicho kwa ajili ya kuendelea na uzalishaji wa bidhaa zao zinaendelea kutolewa. Kwa upande wa Pemba matengenezo madogo yamefanyika katika kituo cha Pujini. Aidha Wakala imeratibu na kuendesha mafunzo ya wajasiriamali kwa mashirikiano na ufadhili kwa wadau wa maendeleo mbalimbali kama Mkuu wa Wilaya Magharibi "A", KOICA, UNDP, TIRDO, Umoja wa Wanawake Kichama, Atiq-aquatic na ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira.

77. **Mheshimiwa Spika,** SMIDA kwa kushirikiana na UNIDO wamewapatia ufadhili wajasiriamali 10 ambao walishiriki katika maonesho ya sabasaba ya 45 jijini Dar es Salaa. Kupitia maonesho hayo washiriki waliweza kufanya mauzo ya zaidi ya T.sh Milioni 20 na kupata oda ya zaidi ya shilingi milioni 35. Aidha, SMIDA imefanya ufuatiliaji wa hati ya makubaliano baina ya SMIDA na TYLLIUM kwa ajili ya mradi wa kuongeza thamani zao la Dagaa.

78. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji SMIDA imewapatia watendaji 4 mafunzo ya muda mfupi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Wafanyakazi 2 walipatiwa mafunzo ya mipango na bajeti, 1 uchambuzi wa taarifa na 1 mafunzo ya kaizen yanayohusu uendeshaji wa ofisi na viwanda. Aidha, tathmini ya utendaji kwa wafanyakazi imefanyika na taarifa ya tathmini hiyo imeandaliwa, sambamba na kukamilisha marekebisho ya muundo mpya wa utumishi na wa taasisi.

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

79. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Biashara pamoja na taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo

ya Viwanda. Programu hii inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Ukuzaji wa Masoko na Usafirirshaji; Uwezeshaji Biashara; na Utengamano wa Biashara na ilipangiwa jumla ya Shilingi bilioni 13.79 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii kuu imeingiziwa jumla ya Shilingi bilioni 2.91 ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida, sawa na asilimia 21 ya fedha zilizopangwa kwa mwaka. Aidha, Program ndogo hizo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

## Programu Ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji

80. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko. Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha nafasi ya Zanzibar ya usafirishaji wa bidhaa katika Masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa. Huduma ambayo inasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Kuongeza Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara.

Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 4.64** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 501.57** kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na **asilimia 11**

ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma za program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

### *Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara*

81. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea na kuangalia mwenendo wa masoko kwa bidhaa nchini pamoja na kuangalia changamoto zilizopo. Kazi hii ilikwenda sambamba na jitihada ya Wizara za kuweka mikakati kwa bidhaa zetu ili tuweze kufikia ushindani katika masoko ya Kanda na Kimataifa ikiwemo ya Afrika Mashariki, SADC, pamoja na kuweza kutanua ushindani kwa soko pamoja la AfCFTA, AGOA na kwengineko Duniani.

82. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu na kushiriki maonesho ya kibiashara ya kimataifa ya Expo Dubai, 2020 na kuzishirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali na wajasiriamali ili kuweza kuwapatia fursa mbalimbali za kutangaza bidhaa na huduma pamoja na kuwasilisha miradi mbalimbali ya maendeleo na uwekezaji nchini. Jumla ya miradi mitano iliwasilishwa katika Maonesho hayo, miradi hiyo ni Ujenzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Kumbi za mikutano na Maonesho, Maeneo ya uwekezaji wa Viwanda, mradi wa Mwangapwani, Bwawani na Uwanja wa Ndege wa Pemba.

83. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu msafara ya kibiashara wenye lengo la kuwapatia fursa za masoko wajasiriamali kwa bidhaa wanazozalisha, ambapo jumla ya wajasiriamali 46 walishiriki katika maonesho ya Jua Kali yaliyofanyika Mwanza Tanzania bara. Uratibu wa msafara huu ulifanyika kwa mashirikiano baina ya Wizara ya Biashara na na Maendeleo ya Viwanda na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

84. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi wa Julai 2021 na jumla ya washiriki 59 kutoka Zanzibar walishiriki katika maonesho hayo. Miongoni mwa washiriki hao, 45 ni Wajasiriamali na 14 ni taasisi za Serikali pamoja na kampuni binafsi. Bidhaa zilizopelekwa na walioshiriki katika maonesho hayo ni pamoja na bidhaa za kusindika, kazi za mikono, nguo, vitenge, sabuni, dawa za asili, bidhaa za viungo (spices), mafuta ya mimea na nyenginezo. Aidha, Maonesho ya Sabasaba yaliweza kutoa fursa kwa wajasiriamali wetu kutangaza bidhaa zao na kuweza kupata wateja wengi zaidi. Kati ya wajasiriamali hao baadhi yao wamepata soko (order) ya kuuza bidhaa zao kwa wateja mbali mbali ikiwemo maduka na 'supermarket'. Jumla ya 'order' 105 zimepatikana kwa wajasiriamali 25 ambao wameendelea kufanya biashara baada ya kumalizika kwa maonesho hayo.

85. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa wafanyabiashara na wajasiriamali wanaweza kupata masoko ya uhakika ya bidhaa zao, Wizara ilitaratibu na kutayarisha Tamasha la nane (8) la Biashara, 2022 ambalo hufanyika kila mwaka ifikapo Januari ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka huu Tamasha hili lilikuwa ni la nane (8) ambalo lilijumuisha jumla ya washiriki 374 kati ya hao 77 ni Taasisi za Serikali, 24 kampuni kubwa, 273 ni wafanyabiashara. Miongoni mwa wafanyabiashara hao, washiriki watano (5) kutoka Kenya, wanne (4) kutoka Burundi, mmoja (1) kutoka Zambia, mmoja (1) kutoka Misri na washiriki ishirini na tano (25) kutoka Uganda. Aidha, kupitia Tamasha la 8 la biashara, Wizara iliandaa siku maalum zikiwemo za Ubunifu, Uchumi wa buluu, Mazingira na vijana. Lengo kuu la kuweka siku hizo ni kuwakutanisha watumiaji, wazalishaji wa bidhaa pamoja na Taasisi zinazohusika na masuala ya biashara na uzalishaji kufanya majadiliano, kuibua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na wazalishaji, na kutoa mapendekezo katika kuimarisha sekta ya biashara na uzalishaji nchini.

86. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha maeneo ya Maonesho ya bidhaa zinazozalishwa na Wajasiriamali wetu, Wizara imeanza hatua ya kutayarisha eneo maalum la kudumu kwa ajili ya kufanyia maonesho na matamasha mbali mbali ya biashara lengo ni

kuhakikisha kuwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara wanapata masoko ya bidhaa zao. Wizara imesaini hati ya makubaliano (MOU) na Kampuni ya ELSEWEDY Electric ya misri ambayo imeonyesha nia ya kushirikiana nasi kuliendeleza eneo hilo.

## Programu Ndogo ya Uwezeshaji Biashara

87. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko pamoja na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Biashara. Programu hii ndogo ina lengo kuharakisha utoaji wa bidhaa na kuboresha taratibu za utoaji mizigo pamoja na kupunguza taratibu, gharama na muda wa usafirishaji na uingizaji bidhaa nchini. Huduma ambazo zinasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Uimarishaji na Uwezeshaji Biashara; Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali; Uimarishaji wa Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji; Usikilizaji na Utoaji wa Maamuzi ya Rufaa za Ushindani zinazotokana na Mamlaka za Uthibiti; Uimarishaji wa Majadiliano ya Kibiashara Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Usimamizi wa Mamlaka zinazotoa Leseni; Uandaaji wa Viwango na Tathmini ya Ubora; na Utoaji Huduma ya Ulinganishi na Matumizi sahihi ya Vipimo. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Shilingi bilioni 9.04** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla

ya **Shilingi bilioni 2.40** kwa ajili ya mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida sawa na **asilimia 27** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma za program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

***Uimarishaji na Uwezeshaji Biashara***

**88. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko yenye lengo la kusimamia na kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara Zanzibar.

**89. Mheshimiwa Spika,** Kupitia huduma hii Wizara ya Biashara imeendelea na kazi ya kufanya mapitio ya Sheria na kanuni za biashara kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa masuala ya biashara ya huduma nchini. Aidha, katika kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara, Wizara imefanya mapitio ya daftari maalum la wafanyabiashara (business directory) ambalo limekusanya taarifa za Wafanyabiashara walioko nchini wakiwemo wazalishaji, watoa huduma na wajasiriamali ambao tayari wamesajiliwa katika mfumo wa Usajili wa biashara. Daftari hilo linatoa fursa kwa wananchi kufahamu biashara zilizopo nchini, huduma zinazotolewa na maeneo wanazotoa huduma hizo.

90. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa uendeshaji wa biashara unaenda sambamba na matakwa ya sheria za usimamizi wa biashara nchini, Wizara ya Biashara imefanya ukaguzi katika maeneo ya wafanyabiashara wanaoingiza na kusafirisha bidhaa kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi. Kupitia ukaguzi huo, wafanyabiashara 120 wamepatiwa hati za usajili wa biashara (Import /Export Registration Certificate) kwa mwaka huu. Sambamba na hilo, Wizara ya Biashara imefanya ukaguzi katika kampuni zinazomilikiwa na wageni au ambazo zimeajiri wafanyakazi wa kigeni kwa lengo la kujua uwepo na maendeleo ya biashara na huduma wanazozitoa kwa kampuni hizo kabla ya kuwaombea vibali vya kufanya kazi nchini. Kwa mwaka 2021/2022, Wizara imewaombea ruhusa kwa taasisi husika ya kupatiwa vibali vya kufanyakazi wafanyabiashara wa kigeni 66 ambao wamewekeza shughuli za kibiashara nchini.

91. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango pamoja na Ofisi ya MKURABITA Tanzania Bara imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 50 walioko katika Wilaya ya Kusini Unguja. Mafunzo hayo yamewalenga wajasiriamali kupata uwelewa kuhusiana na umuhimu wa kusajili biashara zao ili kuweza kutambulika kisheria na kuweza kupata fursa zinazopatikana katika kuendesha biashara katika mfumo rasmi, kuweka kumbukumbu za

biashara zao na umuhimu wa kuwa na akaunti maalum za biashara zao. Aidha, Wizara imeweka kituo jumuishi cha urasimishaji biashara kwa mkoa wa Kaskazini Unguja ambacho kipo Baraza la Mji Mkokotoni, lengo la kituo hicho ni kutoa fursa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara kurasimisha biashara zao kutoka mfumo usio rasmi na kuwa mfumo rasmi. Wizara, kwa sasa inaendelea na taratibu za kuweka kituo cha urasimishaji katika wilaya ya Chake chake Pemba.

***Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali***

92. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Wakala wa Usajili Biashara na Mali (BPRA) yenye lengo la kufanya usajili wa biashara na mali ikijumuisha hati za mali bunifu pamoja na usajili wa nyaraka mbali mbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2021/2022 BPRA imeweza kusajili Kampuni 1,098, Majina ya biashara 1,088, Alama za Biashara 647 na Nyaraka 3,613.

93. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 BPRA ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 988.5** kwa ajili ya mshahara na matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 BPRA imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 445.2** sawa na **asilimia 45** ya makadirio ya mwaka. Aidha BPRA ilipangiwa

kukusanya mapato ya **Shilingi milioni 766.9** kutokana na vyanzo vyake vya mapato, hadi kufikia tarehe 31 Machi, BPRA imeweza kukusanya **Shilingi milioni 973. 8** sawa na **asilimia 126** zilikusanywa na kuingizwa katika mfuko mkuu wa serikali.

94. **Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya mapitio ya sheria, BPRA, tayari imewasilisha rasimu ya sheria ya ufilisi katika Tume ya kurekebisha sheria kwa ajili ya hatua zaidi, sheria ya ubia imewasilishwa serikalini katika ngazi ya makatibu wakuu na sheria ya Nyaraka tayari ishapitiwa Tume ya kurekebisha sheria na imetolewa maoni ya kufanyiwa kazi na BPRA.

95. **Mheshimiwa Spika,** BPRA imetoa matangazo ya usajili wa marudio kupitia vyombo mbalimbali na mitandao ya kijamii (TBC, ZBC TV, gazeti la Zanzibar leo na Mwananchi Communication) kwa kuzitaka kampuni zote zilizoanzishwa Tanzania bara na kupewa hati ya kukidhi Matakwa Zanzibar zinatakiwa kusajiliwa upya kutokana na marekebisho ya kifungo cha 238 cha sheria ya kampuni Nam.15 ya mwaka 2013 yaliofanywa chini ya kifungo 29 ya sheria ya fedha Nam 3 ya mwaka 2021. Aidha, BPRA kupitia maonyesho ya Tamasha la nane la biashara lililofanyika Maisara imetoa elimu kwa wananchi na wafanya biashara mbalimbali juu ya usajili wa biashara na mali kwa maendeleo yao na Taifa.

96. **Mheshimiwa Spika,** Wafanyakazi 8 wa BPRA wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi, Mafunzo hayo ni ya kujenga uelewa wa mfumo wa biashara na upokeaji malalamiko kielektroniki. Mafunzo elekezi kuhusu Usajili wa Bidhaa katika Eneo huru la Biashara la Bara la Afrika. Pia mafunzo ya uchambuzi wa taarifa na ya mfumo mpya wa Bajeti. Aidha, BPRA imefanya safari 7 za kikazi, 4 za kikazi Pemba na safari 2 Dar es salaam katika maonyesho ya sabasaba na kikao na NIDA cha kutumia njia mpya za taarifa na safari 1 Morogoro katika kushiriki kikao cha kazi cha wadau kwa ajili ya kujadili ripoti ya tathmini ya jukwaa la kimataifa la kubadilishana taarifa za kodi.

***Uimarishaji wa Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji***

97. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji (ZFCC) chini ya sheria namba 5 ya mwaka 2018 yenye lengo la kuhamasisha, kuimarisha na kulinda ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji hapa Zanzibar kwa kuhakikisha kwamba kila muekezaji, mwenye kiwanda, Mfanyabiashara na Mjasiriamali anafanya shughuli zake bila ya kumkwaza mwengine kwa ajili ya ustawi wa wananchi na uchumi wa Zanzibar.

98. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ZFCC ilipangiwa jumla ya Shilingi milioni 236.4 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 ZFCC imeingiziwa jumla ya Shilingi milioni 85.0 sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka. Aidha ZFCC ilipangiwa kukusanya mapato ya Shilingi milioni 583.02 kutokana na chanzo chake cha mapato, hadi kufikia tarehe 31 Machi, ZFCC imeweza kukusanya Shilingi milioni 820.64 sawa na asilimia 140 na kuziingiza katika mfuko mkuu wa serikali.

99. **Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia vema jukumu la ushindani halali wa kibiashara ZFCC kwa mwaka wa fedha 2021/20222 imeidhinisha jumla ya miungano saba (7) ya Makampuni kati ya hiyo miungano miwili (2) imeidhinishwa kwa masharti ya kusimamia ushindani na mitano (5) imeweza kuridhiwa bila ya masharti. Aidha, ZFCC imepokea malalamiko manne (4) kutoka kwa wafanyabiashara na yamefanyiwa kazi kwa kufikishwa mbele ya Tume na kutolewa maamuzi stahiki.

100. **Mheshimiwa Spika,** Katika kulinda afya ya mlaji kwa bidhaa zilizopo Zanzibar, Wizara ya Biashara kupitia ZFCC imefanikiwa kukagua maduka 1,527, Maghala 29 na Maduka Makubwa (Supermarket) 14. Katika ukaguzi huo bidhaa bandia na zilizopitwa na muda wa matumizi zimekamatwa zikiwemo za

umeme, vifaa vya simu aina ya Samsung, Vyakula vya makopo, Kemikali na bidhaa za matumizi ya nyumbani. Pamoja na kufanya uteketezaji wa bidhaa ya tende iliyopitwa na muda wa matumizi na haifai kwa matumizi ya binadamu jumla ya vipolo nane (8) vyenye kilo 25 kwa kila kimoja viliteketezwa.

**101.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imewakamata wafanyabiashara wa jumla na rejareja kwa kosa la kutokuweka utambulisho wa bei elekezi (Price display), kuuza bidhaa zilizopitwa na muda wa matumizi na kukiuka bei elekezi kwa bidhaa muhimu ya unga wa ngano, sukari, mafuta na mchele. Sambamba na kuuza bidhaa ya saruji kinyume na bei elekezi iliyowekwa na Serikali. Katika makosa hayo, jumla ya **TZS 76,425,000** zilikusanywa na kuingizwa katika mfuko mkuu wa serikali.

**102.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kumlinda mtumiaji kwa watoa huduma Wizara kupitia ZFCC imefanya ukaguzi wa mikataba 58 ya Benki kwa ajili ya kuisajili kisheria. Katika ukaguzi huo tumefanikiwa kuondoa masharti kandamizi yanayomkandamiza mtumiaji na baadhi yao waliweza kupatiwa vyeti vya usajili wa mikataba. **Kiambatanisho namba 4** kinaonesha Benki zilizopatiwa vyeti vya usajili.

***Usikilizaji na Utoaji wa Maamuzi ya Rufaa za Ushindani zinazotokana na Mamlaka za Uthibiti***

**103. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Baraza la Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar (Zanzibar Fair Competition Tribunal - ZFCT) ni taasisi ya kisheria iliyoundwa ndani ya sheria namba 5 ya mwaka 2018 chini ya kifungu cha 26, yenye lengo la kuimarisha udhibiti wa vitendo vinavyokwenda kinyume na kuathiri ushindani wa biashara na kumlinda mtumiaji wa bidhaa na huduma ndani ya Zanzibar.

**104. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ZFCT ilipangiwa jumla ya Shilingi milioni 390.0 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 ZFCT imeingiziwa jumla ya Shilingi milioni 68.3 sawa na asilimia 18 ya makadirio ya mwaka.

**105. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha uthibiti wa vitendo vinavyokwenda kinyume na ushindani wa biashara unasimamiwa vizuri, Wizara kupitia ZFCT imefanya vikao viwili vya kusikiliza shauri la rufaa baina ya kampuni ya La Rosa Dei Venti Limited na Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar. Aidha, ZFCT imepokea indhari ya rufaa (Notice of Appeal) iliyokatwa na Zanzibar Milling Corporation

LTD dhidi ya Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kuhusiana na maamuzi ya bei elekezi ya unga wa ngano. Hata hivyo, mrufani huyo hakuendelea na utaratibu wa kukata rufaa.

106. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza mkakati wa mawasiliano, ZFCT imeandaa kipindi 1 cha Televisheni na Maelezo baada ya Habari kwa kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), imetoa Mafunzo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu mbali mbali vya Zanzibar waliohudhuria katika Jukwaa la Mtumiaji Tanzania (TCF) katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakil ambayo yalirushwa na SN TV online, kutoa elimu kwa Mawakili kupitia mkutano mkuu wa Jumuia ya Mawakili Zanzibar (ZLS) na kuandaa kongamano moja (1) la kuitangaza ZFCT kwa wadau wake kwa kuwakutanisha wadau kutoka sekta Binafsi na za Serikali.

107. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi, Wizara kupitia ZFCT imekamilisha kanuni za ZFCT kwa mujibu wa sheria pamoja na kufanya tafsiri ya Kiswahili ya Kanuni hizo na muongozo wake. Aidha, muundo wa utumishi wa ZFCT umekamilika na kuidhinishwa wenye sura ya Baraza, Mrajis, Idara na vitengo. Pia, ZFCT imewajengea uwezo wafanyakazi saba (7) na wajumbe wake wane (4) juu ya Sheria ya Ushindani

kwa njia ya Mtandao yaliyoendeshwa na Ubunifu initiative kwa kushirikiana na Tanzania Law Society, mafunzo ya mapatano juu ya Uwekezaji, Malibunifu na Sheria ya Ushindani, mafunzo ya Mikataba inayohusiana na manunuzi ya Umeme (Power Purchase Agreement) na mafunzo ya namna ya kuunda na kutumia mfumo wa Indeksia wa Majalada (Keyword Filing System).

**108.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha uwelewa wa wananchi juu ya uwepo wa ZFCT kisheria unaongezeka, ZFCT imeshiriki maonesho ya nane (8) ya Biashara ambayo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya kazi zinazotekelezwa na Baraza hilo.Vile vile, ZFCT imeshiriki katika siku ya Mtumiaji Duniani ambapo maadhimisho hayo kitaifa yalifanyika Zanzibar tarehe 15 Machi, 2022 pamoja na kushiriki katika wiki ya ushindani iliyozinduliwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda tarehe 6 Disemba 2021.

***Uimarishaji wa Majadiliano ya Kibiashara Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi***

**109.** **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC) chini ya sheria namba 10 ya mwaka 2017 yenye lengo la kuandaa majadiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta

Binafsi ili kutatua changamoto zinazoikabili sekta kuu za uchumi. Jukwaa hilo inaleta faida kubwa katika kukuza biashara na utoaji wa huduma pamoja na kuondoa changamoto mbali mbali za kibiashara zinazozikabili pande hizo mbili. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ZNBC ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 326.9** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 ZNBC imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 68.7** sawa na asilimia 21 ya makadirio ya mwaka.

**110. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini sana mchango wa sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi, na ndio maana tunaitambua sekta hiyo kama ndio injini ya uchumi wa Zanzibar. Katika kufikia lengo la kutungwa kwa Sheria hiyo ya Baraza, Mabaraza ya Biashara ya Mikoa pamoja Kamati za Baraza la Taifa yameundwa ili kuweza kushughulikia changamoto ambazo zinajitokeza pale ambapo Baraza la Taifa halikuweza kukutana.

**111. Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara, kupitia Baraza la Taifa la Biashara imefanya mazungumzo na Trade Mark East Africa (TMEA) kuweza kulisaidia Baraza la Taifa la Biashara kuweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa

Sheria. Katika kutekeleza makubaliano hayo, TMEA wameanza kuijengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo ya kuweza kujadiliana wataalamu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara (ZNCC) pamoja na wale wa Baraza.

112. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa, jumla ya mikutano minne ya Mabaraza hayo imefanyika. Masuala yaliyojitokeza katika mikoa hiyo ni pamoja na changamoto za tofauti ya bei za bidhaa baina ya Unguja na Pemba ambapo wajumbe wa Mabaraza ya Biashara waliomba kuwekwa miundo mizuri ya Bandari za Pemba ili kuweza kupokea shehena za mizigo kutoka nje moja kwa moja kisiwani humo. Aidha, Mabaraza hayo yalipendekeza kufanyiwa marekebisho kwa Sheria Nam. 10 ya mwaka 2017 ili kuweka kifungu kitakacho wawezesha Mabaraza hayo kuweza kutafuta vyanzo vyao vya fedha. Masuala yaliyowasilishwa yanaendelea kufanyiwa kazi na Baraza la Taifa ili kuweza kuwasilisha Marekebisho hayo ya Sheria mbele ya Baraza lako hili.

113. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Biashara lina jumla ya Kamati nne (4) ambazo ni: Kamati ya Uchumi, Biashara, Kodi na Uwekezaji; Kamati ya Kilimo, Uvuvi, Mifugo na Mazingira; Kamati ya Utalii na Kamati ya Ajira. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miezi tisa, Kamati mbili zilikutana.

Kamati hizo ni ile inayoshughulikia uchumi pamoja na ile ya masuala ya Ajira. Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na uimarishaji wa majadiliano ya masuala ya ajira baina ya serikali, waajiri na waajiriwa (social dialogue); kufanya mapitio ya mafao yanayotolewa katika mfuko wa hifadhi ya jamii Zanzibar (ZSSF) ili kuongezwa masuala ya haki za kutokuwa na ajira (Unemployment benefit); kuangaliwa upya viwango vinavyotozwa kwa ajili ya kodi ya kuendeleza ujuzi kwa vijana (skills development levy – SDL) ili kuweza kupunguzwa kutoka asilimia 5 ya sasa na kuwekwa asilimia 4 na pia kuangalia jinsi ya kuweza kurejesha kiwango kidogo cha tozo hiyo kwa sekta binafsi;

Aidha, Jumuiya ya ZATO iliwasilisha mapendekezo ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato yanayotolewa katika maeneo ya vivutio vya utalii mbele ya Kamati ya Uchumi, Biashara, Kodi na Uwekezaji na kujadiliwa. Kamati ndogo inayoongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nchi Fedha na Mipango iliundwa kwa ajili ya kuupitia mfumo ili kujua faida na hasara zake kabla ya kukubalika kutumika rasmi.

114. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Baraza liliandaa kikao cha pamoja baina ya wafanyabiashara na Bodi ya Mapato ya Zanzibar - ZRB, ili kujadili kwa pamoja changamoto ambazo zilijitokeza za utumiaji wa

mashine za VFMS. Baada ya kikao hicho wadau walikubaliana kwamba kuna haja ya kutolewa elimu zaidi kwa wafanyabiashara ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utumiaji wa mashine hizo mpya za utoaji wa risiti. Aidha, kikao hicho kiliwasihi wafanyabiashara kutii agizo la Serikali na kuendelea kutoa risiti kila pale wanafanya mauzo ya bidhaa zao.

***Usimamizi wa Mamlaka zinazotoa Leseni***

**115.** **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni (BLRC) chini ya sheria namba 13 ya mwaka 2013 yenye lengo la kusimamia mfumo wa utoaji leseni na tozo kwa Mamlaka za Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 BLRC ilipangiwa jumla ya **Shilingi milioni 347.4** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 BLRC imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 77.4** sawa na asilimia 22 ya makadirio ya mwaka.

**116.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Baraza liliweka vipaumbele ambavyo ni kusimamia na kuratibu matumizi ya mfumo wa utoaji leseni (NOBS) utakaohusisha Mamlaka za Utoaji leseni ili kurahisisha upatikanaji wa leseni kwa wafanyabiashara pamoja na kuondosha urasimu

kwa kufanya mapitio ya taratibu, gharama na muda wa upataikanaji wa leseni. Katika kulitekeleza hilo, Wizara kupitia BLRC imezihakiki taarifa za leseni za Mamlaka zinazohusiana na sheria, aina ya leseni, mahitaji, ada, muda wa utoaji leseni ili ziendane na mfumo (NOBS) na kutoa mafunzo ya mfumo huo kwa Mamlaka 26 za utoaji wa leseni.

117. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuondosha urasimu BLRC kwa kushirikiana na Shirika la Bandari (ZPC) imeratibu uanzishaji wa kituo jumuishi Bandarini (one stop center) ambapo Mamlaka zote zinazohusika na utoaji mizigo zitakaa sehemu moja pamoja na uanzishaji wa mfumo wa pamoja wa utoaji mizigo bandarini ili kuondosha usumbufu kwa wafanyabiashara kupita katika ofisi tofauti kupata huduma. Aidha, BLRC kwa kushirikiana na ZEMA imeunganisha ada na kuweka Utaratibu mpya wa malipo ya ada za vyeti vya kimazingira ukijumuisha na gharama za mchakato wa upatikanaji wa vyeti hivyo badala ya kufanya malipo tofauti. BLRC pia kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii (ZCT) imekusanya taarifa za mahoteli 646 za utoaji wa leseni, vibali na ada zinazotozwa na Mamlaka (12) zinazohusika na uendeshaji wa mahoteli ili kuanza utaratibu wa utoaji wa leseni na malipo kufanyika sehemu moja na mamlaka kugawana mapato yao.

**118. Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Katika kuimarisha mazingira ya Biashara nchini, Wizara imefanya Tathmini ya mazingira ya biashara (Zanzibar Business Enabling Environment) kwa mwaka 2021 kwa kuzingatia vigezo 17 kati ya hivyo vigezo 10 vinatumiwa na Benki ya Dunia na vigezo saba (7) vimetumika kulingana na mazingira ya biashara ya Zanzibar. Kiujumla tathmini imeonesha kwamba Zanzibar imeshika nafasi ya 94 kati ya nchi 191 iliyojilinganisha nazo kwa kupata alama 63.2 na nafasi ya tano (5) kwa nchi za visiwa. Aidha, Matokeo yanaonesha kwamba Zanzibar imepiga hatua katika urahisi wa ufanyaji biashara na kuingia katika kundi la nchi zenye mazingira mazuri ya biashara kwa sifa maalum (Most notable improvement business environment) kutokana na kufanya mageuzi (reforms) kwa maeneo mbalimbali.

### *Uandaaji wa Viwango na Tathmini ya Ubora*

**119. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) chini ya sheria namba 1 ya mwaka 2011 yenye lengo kusimamia uanzishwaji na usimamizi wa viwango kwa huduma na bidhaa. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ZBS ilipangiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 6.15.** Kati ya fedha hizo Shilingi Milioni 841.3 kwa ajili ya mishahara, **Shilingi Milioni 305.5** kwa kazi

za kawaida na **Shilingi Bilioni 5.0** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 ZBS imeingiziwa jumla ya **Shilingi Bilioni 1.49** sawa na asilimia 24 ya makadirio ya mwaka. Aidha ZBS ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi milioni 702.7** kutokana na chanzo chake cha mapato, hadi kufikia tarehe 31 Machi, ZBS imeweza kukusanya **Shilingi milioni 595.3** sawa na **asilimia 85** kwa makadirio ya mwaka  na kuziingiza katika mfuko mkuu wa serikali.

**120.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara imeendelea kusimamia vyema suala la kuendeleza viwango kwa kuhakikisha tunaweza kuwa na viwango kwa bidhaa na huduma vya kutosha na kuweza kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara wetu. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara kupitia ZBS imeweza kuandaa jumla ya viwango 106 sawa na asilimia 118 ya lengo la uandaaji viwango 90 kwa mwaka husika.  Viwango vilivyoandaliwa ni pamoja na:- Viwango 40 vya bidhaa za chakula;  viwango 25 vya bidhaa za kemikali; Viwango 22 vya bidhaa za Uhandisi Mitambo na Vyombo vya Moto; Viwango 10 vya Mazingira; Viwango 4 vya huduma za utalii; na Viwango 5 vya bidhaa za umeme na elektroniki.

**121.** **Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa kazi za uandaaji wa viwango Wizara imeshiriki katika

mikutano inayohusiana na uandaaji wa viwango ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha kuwa matakwa ya wadau wa Zanzibar yanawasilishwa na kujumuishwa ipasavyo. Mikutano na Semina zilizohudhuriwa ni pamoja na kamati za kitaalam za kuandaa viwango vya samaki, maziwa na viungo. Maelezo zaidi ya vikao vilivyohudhuriwa vinaonekana katika kiambatanisho namba 5.

**122. Mheshimiwa Spika,** Suala la usimamizi wa ubora ni suala nyeti na limewekewa mikakati ambayo utekelezaji wake unakwenda sambamba na malengo yaliowekwa. Katika kutekeleza hilo, Wizara ya Biashara kupitia ZBS imeweza kutoa leseni za Alama ya Ubora 23 ambapo ni sawa na **asilimia 48** ya lengo la leseni 48 zilizopangwa kwa mwaka. Leseni 18 za Alama ya Ubora zilitolewa kwa bidhaa 18 ambazo zimethibitishwa kwa utaratibu wa kutumia Viwango vya Zanzibar (ZBS Standard Mark) na bidhaa tano (5) zimethibitishwa kwa utaratibu wa kutumia viwango vya visivyo kuwa vya Zanzibar (Tested Product Certificate).

**123. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia suala la uchunguzi wa Maabara Wizara kupitia ZBS imefanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli 622. Kati ya hizo Sampuli 70 ziliwasilishwa maabara za umeme, sampuli 280 maabara ya chakula na sampuli 272

maabara ya kemikali. Aidha, matokeo ya ripoti hizo za uchunguzi wa kimaabara kwa bidhaa yanaonyesha kwamba sampuli za bidhaa 584 zimekidhi vigezo vya viwango kwa bidhaa husika na sampuli za bidhaa 38 zimebainika kutokidhi vigezo vya viwango husika. Pia, ZBS imefanya ukaguzi kwa shehena za bidhaa nyenginezo (General goods) 932 kupitia mfumo wa ukaguzi nje ya nchi (PVoC) na shehena za bidhaa 3,053 zimekaguliwa kupitia mfumo wa ndani ya nchi (DI) na kupatia vyeti vya ubora.

**124. Mheshimiwa Spika,** Vile vile, ZBS imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Ofisi na maabara katika eneo la Maruhubi na uzinduzi wake umefanyika tarehe 09 Januari 2022 na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed S. Abdulla. Hatua inafuata ni kukamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara ili bidhaa zaidi zifanyiwe uchunguzi hapa hapa Zanzibar.

***Utoaji Huduma ya Ulinganishi na Matumizi sahihi ya Vipimo***

**125. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii inatekelezwa na Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) chini ya sheria namba 6 ya mwaka 2020 yenye lengo la kuhakikisha majibu ya vipimo katika miamala ya

biashara yanafanyika kwa usahihi pamoja na kufanya uhakiki wa vipimo.

**126.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ZAWEMA ilipangiwa jumla ya Shilingi milioni 530.5 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022 Wakala imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 164.4** sawa na asilimia 31 ya makadirio ya mwaka. Aidha ZAWEMA ilipangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi milioni 179.7** kutokana na chanzo chake cha mapato, hadi kufikia tarehe 31 Machi, ZAWEMA imeweza kukusanya **Shilingi milioni 154.8** sawa na **asilimia 86.1** ya makadirio ya mwaka na kuziingiza katika mfuko mkuu wa serikali.

**127.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha ulinganishi wa vipimo uko sahihi kwa mujibu wa mahitaji ya wananchi, Wizara kupitia ZAWEMA imefanya uhakiki wa nyenzo za kufanyia kazi (Standard Equipment) 48 Unguja na Pemba. Aidha, ZAWEMA imefanya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kufanyia kazi .

**128.** **Mheshimiwa Spika,** ZAWEMA kwa kushirikiana na Wakala wa Vipimo Tanzania imeshiriki katika Tamasha la nane (8) la Biashara Maisara kwa lengo la kujitangaza na kutoa elimu kwa jamii inayohusiana na umuhimu wa vipimo na uhakiki. Pia, ZAWEMA

imefanya kikao na wadau wa vipimo na wameweza kushiriki katika safari 3 za kimafunzo.

**129.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (ZAWEMA) imefanya uhakiki wa gari 20 za kusambazia mafuta, Matangi ya kuhifadhia mafuta 53, uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa 35, uhakiki wa mita 427 za vituoni, uwanja wa ndege 18 na 15 mita za bohari pamoja na upimaji wa mafuta yanayoingizwa nchini jumla ya lita 55,682,566. Pia, ZAWEMA imefanya uhakiki wa mizani 1,828 katika Shehia mbalimbali.

## Programu Ndogo ya Utengamano wa Kibiashara

**130.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko. Programu hii ndogo ina lengo kuimarisha biashara huria inayopelekea upanuzi wa soko na kuongeza biashara baina ya nchi na nchi. Huduma ambayo inasimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni Uimarishaji wa Utengamano wa Kibiashara.Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya Shilingi milioni 108.09 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi 2022, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **Shilingi milioni 9.16** kwa ajili kazi za kawaida sawa

na asilimia 8 ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma za program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

**Uimarishaji wa Utengamano wa Kibiashara**

**131. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika hatua ya kuimarisha Mashirikiano ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa imeweza kushiriki katika mikutano mbali mbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na masuala ya biashara. Mikutano hiyo ni pamoja na vikao vya majadiliano ya uanzishwaji wa eneo huru la biashara barani Afrika (Continental Free Trade Africa) ambapo Tanzania tayari imesharidhia utekelezaji wa Mkataba huo; Vikao vya itifaki ya biashara ya huduma Afrika Mashariki; Vikao vya kujadili kuondosha vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru (Non Tariff Barriers- NTBs); Vikao vya urahisishaji biashara (Trade Facilitation); Vikao vya usimamiaji wa masuala ya Vikwazo vya Kiufundi vya Kibiashara (Technical Barriers to Trade-TBT) na masuala ya afya ya Wanyama na Mimea (Sanitory and Phyto Sanitory- SPS); Vikao vya SADC. Lengo la ushiriki wa vikao hivi ni kuweza kuhakikisha mazingira ya ufanyaji biashara yanakuwa rafiki katika masoko ya Ndani, Kikanda na Kimataifa.

**132. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia idara hii imefanya ziara 2 za kikazi Tanzania bara ambazo zilihusiana na Maandalizi ya Mkutano wa mwaka wa Uwekezaji unaotarajiwa kufanyika Dubai, Vikao

vya Maandalizi vya mkutano wa bilateral baina ya Tanzania na Kenya, ziara katika vituo jumuishi vya urasimishaji biashara Moshi na Arusha.

## 5. SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

133. **Mheshimiwa Spika,** Shirika kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika (Corporate Strategic Plan) wa miaka mitano 2021-2025 pamoja na mpango wa biashara wa miaka mitano 2021-2025. Kwa mwaka huo, Shirika lilikabiliwa na msimu mkubwa wa vuno la Karafuu na kupelekea utekelezaji wa mipango yake kutekelezeka kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, Shirika liliendelea kuimarisha bidhaa linazozalisha, kuimarisha majengo kwa lengo la kuongeza kipato na kuhuisha ustawi wa Shirika.

134. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kukusanya mapato yanayotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo mauzo ya karafuu na mafuta ya mimea, mapato yanayotokana na majengo na mapato mengineyo. Kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 Shirika lilipanga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 91.2 hadi kufikia tarehe 10 Machi, 2022 Shirika limeweza kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 136.7 ambapo ni sawa na asilimia 150 ya makadirio kwa

mwaka. Sababu ya kuongezeka kwa mapato hayo, kunatokana na msimu mkubwa wa karafuu kinyume na matarajio yaliyowekwa pamoja na bei ya kuuzia karafuu kuongezeka katika soko la dunia.

**135.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2021/2022 Shirika lilijipangia kununua tani 5,630 za karafuu kavu kwa gharama ya Shilingi bilioni 56.3 ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi Shirika limeweza kununua tani 8,703 za karafuu kavu kutoka kwa Wakulima kwa gharama ya Shilingi bilioni 113.36. Karafuu zilizonunuliwa ni sawa na asilimia 1584.6 ya makadirio ya kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa ununuzi wa Makonyo Shirika lilijipangia kununua Makonyo tani 1,004.2 kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1.7 hadi kufikia 31 Machi, jumla ya tani 1,744.6 za Makonyo zimenunuliwa zenye gharama ya Shilingi milioni 2.6 sawa na asilimia 146 ya makadirio ya mwaka.

**136.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa ununuzi wa mwani, Shirika kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limenunua **tani 76.69** za mwani kwa gharama ya **Shilingi milioni 59.105** kwa lengo la kuimarisha ukulima wa zao la mwani na upanuzi wa masoko yenye tija. Aidha, bei ya mwani aina ya "Cottonii" kwa kilo 1 umenunuliwa kwa TZS 1,800 na mwani aina ya "Spinosum" ni TZS 700 kwa kilo 1.

**137. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi kirefu sasa Shirika limekuwa likikabiliwa na uhaba wa magunia kwa ajili ya kuhifadhia na kusafirishia karafuu, kwa mwaka 2021-2022 Shirika lilijipangia shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ununuzi magunia, nyuzi za katani na pishi. Hadi kufikia tarehe 31 Machi Shirika limeweza kununua vifaa hivyo kwa thamani ya Shilingi Milioni 873 sawa na **asilimia 60** ya makadirio ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa usafirishaji karafuu Shirika limeweza kusafirisha tani 8,321.61 za karafuu zenye thamani ya **Shilingi bilioni 144.7**.

**138. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kwamba ukulima wa zao la karafuu unaimarishwa kwa maendeleo ya nchi na ustawi wa watu wake, Shirika limekuwa likitoa huduma mbali mbali kwa kushirikiana na Taasisi nyengine ambazo ni Wadau wa karafuu. Katika kuhakikisha kwamba Wakulima wa karafuu wanapatiwa miche bora na kwa wakati, Shirika limetoa **Shilingi milioni 25.2** kwa Wizara inayohusika na Kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa miche hiyo. Aidha, Shirika limeweza kulipa kiasi cha **Shilingi milioni 151.9** kwa ajili ya Kikosi Kazi cha kuzuwia magendo.

**139. Mheshimiwa Spika**, Tawi la ZSTC Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 lilijipangia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 1.4

katika mauzo ya bidhaa zake, hadi kufikia 31 Machi 2022, Tawi limekusanya jumla ya shilingi milioni 703. Makusanyo haya ni sawa na asilimia 49 ya makadirio kwa mwaka. Hata hivyo, kwa upande wa matumizi Tawi lilijipangia kutumia **Shilingi bilioni 1.38**, hadi kufikia 31 Machi, 2022 Tawi limetumia kiasi cha **Shilingi milioni 686.6** ambazo ni sawa na asilimia 49 ya makadirio kwa mwaka. Mapato pamoja na matumizi yameshuka kutokana na kufungwa kwa Duka la Manzese ambalo lilionekana kutokufanya vizuri kutokana gharama za uendeshaji kuwa kubwa.

140. **Mheshimiwa Spika,** Shirika kwa kipindi kirefu limekuwa likifanya utaratibu wa kuweza kulifunga Tawi la Dubai kutokana na kutokuwepo umuhimu wa Tawi hilo kwa sasa. Shirika limeshafanya taratibu ambapo kwa sasa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali pamoja na Mthamini wameenda Dubai kuangalia na kutathmini utaratibu mzima wa Tawi hilo. Aidha, Fedha za Viinua mgongo kwa ajili ya kuwalipa Wafanyakazi wa Dubai tayari zimeshaigizwa katika Akaunti ya Dubai kwa ajili ya kuwalipa. Pia, utaratibu wa kutafuta sehemu ambayo Mali (Assets) za Shirika zitahifadhiwa kwa ajili ya kuuzwa unafanyiwa kazi.

141. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZSTC imeendelea kuimarisha Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo na Arki za Mimea kwa kuanza utaratibu wa kuajiri Kampuni ya Wafanyakazi ambapo tayari mikataba imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ridhaa. Sababu ya kutaka kuajiri ni kutokana na kushuka kwa matumizi ya Kiwanda yaliosababishwa kwa kutokufanya kazi kwa Kiwanda kwa sababu ya upungufu wa nguvu kazi ambapo Wafanyakazi wa Mkataba wamestaafishwa.

## 5. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2021-2022

142. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa malengo na majukumu mbali mbali ya Wizara kwa mwaka 2021/2022, pia zipo changamoto zilizoathiri utekelezaji wa malengo yaliopangwa katika sekta ya Biashara na Viwanda. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Ufinyu wa sehemu zakufanyia kazi: Wizara imeendelea kutumia majengo yaliyopo pamoja na kukodi ofisi kwa baadhi ya Taasisi zake.
ii. Kukosekana kwa wataalam wenye sifa katika baadhi ya Taasisi: Wizara tayari imeomba Serikalini pamoja na kutumia wataalam kutoka nje ya Wizara ikiwemo kutoka Tanzania Bara.

iii. Ukosefu wa eneo la kudumu la kufanyia maonesho na matamasha ya biashara: Wizara inajipanga kuweka miundombinu ya awali ili kuweza kulitumia eneo la Nyamanzi/Dimani kwa maonesho.

iv. Ukosefu wa Soko la Hisa (Stock Exchange Market), kutokana na ongezeko la Kampuni sasa ni muda muwafaka kwa Zanzibar kuwa na soko lake kama ilivyo Tanzania Bara ili wananchi waweze kupata fursa ya kuekeza katika Kampuni kwa kununua hisa kutoka kampuni za umma zitakazo orodheshwa katika soko la Hisa.

## 6. PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023

**143. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika utekelezaji wa majukumu yake imepanga vipaumbele vyake kwa kwenda sambamba na kasi ya Serikali ya awamu ya nane (8) ya kuendeleza viwanda kama ilivyoelezwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2021-2025, Dira ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026), Mpango Kazi wa Ahadi za Mheshimiwa Rais, 2021-2025 pamoja na miongozo na Sera za Wizara. Maeneo mengine makuu yatakaopewa kipaumbele ni pamoja na kuweka mazingira mazuri

ya Biashara, kupanua wigo wa vipimo, utafutaji wa masoko na usaidizi wa wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo.

144. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inatarajia kutekeleza shughuli mahsusi zifuatazo katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/2023:-

**1. Kuendeleza Sekta ya Viwanda:**

145. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza viwanda, Wizara imekusudia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. **Kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda:**
Wizara inatarajia kuyaendeleza maeneo ya Viwanda ya Dunga na Pangatupu kwa kuyapima, kuandaa Mpango wa Matumizi ya ardhi, kulipa fidia kwa wananchi, kufikisha miundombinu ya umeme, maji pamoja na kutengeneza barabara za ndani. Aidha, Wizara itaendeleza juhudi za kutafuta wabia katika kuyaendeleza maeneo haya ya viwanda.

ii. **Kuanzisha na kuendeleza Sekta ya Tehama ya Viwanda:**

Wizara inataanzisha na kuendeleza sekta ya Tehama ya Viwanda ili kuhakikisha wananchi

wanapata taarifa kuhusu shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinatekelezwa katika sekta hii. Aidha, kama inavyojulikana kuwa Teknolojia ya Habari na mawasiliano (Tehama) ni nyenzo muhimu ambayo mchango wake ni mkubwa katika kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya uchumi wa Viwanda.

**iii. Kufanya Sensa ya Viwanda:**

Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda itafanya Sensa ya Viwanda ili kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi ya viwanda vilivyopo Zanzibar. Sensa hii itasaidia kuweza kupanga mipango mbalimbali inayohusu sekta hiyo kwa kuwa na idadi sahihi ya viwanda vilivyopo.

iv. **Uimarishaji wa miundo mbinu kwa wazalishaji na upatikanaji wa huduma za kifedha, masoko na vifungashio:**

Katika kuhakikisha wajasiriamali nchini wanaimarika katika shughuli zao, Wizara kupitia SMIDA itahakikisha inatoa mafunzo ya kutosha kwa wajasiriamali Pamoja na kuwapatia mitaji kupitia mikopo yenye riba nafuu. Aidha, Wizara itahakikisha inatafuta masoko yenye tija kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wetu.

**2. Kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko:**

146. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Biashara, Wizara itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. **Kuendeleza Uwanja wa Kimataifa wa Mikutano na Maonesho wa Zanzibar:**

Wizara tayari imeingia makubaliano (MoU) na Kampuni ya Elsewedy kutoka nchini Misri ili Kujenga na kuliendeleza eneo la Nyamanzi kwa ajili ya mikutano na maonesho ya kimataifa, hivyo juhudi hizi zitaendelezwa.

Vile vile Wizara inakusudia kuandaa eneo kwa ajili ya maonesho ya Biashara Zanzibar yanayofanyika kila mwaka ifikapo Januari. Katika hatua za awali Wizara itaanza na kusafisha eneo, kupeleka miundo mbinu ya maji, umeme na barabara. Aidha, Wizara tayari imewasiliana na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Shirika la Maji Zanzibar (ZAWA) pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa ajili ya kupatiwa huduma katika eneo hilo.

ii. **Kuendelea kuzitafutia masoko bidhaa zinazozalishwa nchini:**

Wizara itaendeleza kushiriki katika majadiliano mbali mbali ya ushirikiano ya kinchi, kikanda na kimataifa pamoja na kushiriki katika maonesho mbalimbali ili kutafuta masoko mapya.

### 3.Kuboresha Mazingira ya ufanyaji biashara na utoaji huduma

**i. Kuandaa na kupitia Sheria na Kanuni:**

**147. Mheshimiwa Spika,** Wizara itafanya mapitio ya Sheria zote zinazosimamiwa na taasisi zilizopo chini yetu ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi kulingana na hali ilivyo sasa. Mapitio ya sheria yatasaidia kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yaliyo chini ya Wizara kwa kuzingatia malengo mahususi ya nchi. Vile vile Wizara inakusudia kutunga sheria mpya ya maendeleo ya viwanda ya Zanzibar pamoja na kanuni mbalimbali.

**ii. Kuimarisha na Kutambulika kwa maabara zilizopo za ZBS (Accreditation):**

Wizara itahakikisha maabara za ZBS zinatambulika kwa kuwapatia mafunzo wataalamu wa maabara, kushiriki katika vikao mbalimbali vya kisekta na kikanda, kuimarisha maabara mpya zilizopo maruhubi kwa kufanya matengenezo na ununuzi wa vifaa vipya vya kisasa.

iii. **Kuweka miundombinu na mifumo ya TEHAMA itakayofanikisha utekelezaji wa kazi:**

Wizara inatarajia kuanzisha mifumo na kuweka miundombinu muhimu wezeshi ya tehama ili kuhakikisha idara na taasisi zake zinafanya na kazi kwa ufanisi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Vile vile, Wizara imejipanga kuondosha urasimu katika utaratibu mzima wa upatikanaji wa utoaji leseni, vibali na ruhusa nyengine za kuendesha biashara pamoja na kufanya mapitio ya ada ili kurahisisha ufanyaji biashara nchini.

iv. **Kufanya Tafiti katika masuala ya Biashara na viwanda,** Wizara itafanya tafiti katika masuala ya Biashara na viwanda ili kuhakikisha Sekta hizi zinazidi kukua na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

v. **Kufanya tafiti na tathmini za mazingira ya ufanyaji biashara:** Wizara itafanya utafiti huu maalum kwa kutumia vigezo maalum vinavyotumiwa na taasisi za kimataifa ili kupima matokeo na kujua maeneo yanayohitajitaji kuimarishwa katika utoaji wa huduma.

vi. **Kuwajengea uwezo Wafanyakazi,** Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo mbali mbali wafanyakazi wake wa Idara, Taasisi na Mashirika ili kuhakikisha kazi zinafanywa kwa weledi ili kufikia malengo yaliyowekwa. Wizara itahakikisha kila taasisi inawapatia watendaji wake mafunzo mahususi kulingana na majukumu ya taasisi husika.

### 4. Kuendeleza Shughuli za Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)

**i. Ununuzi wa Karafuu na Makonyo:**

**148. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) inatarajia kuongeza ununuzi wa karafuu tani 4,000 kwa gharama ya shilingi bilioni 56.0 na Makonyo tani 800 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.2 ili kuhakikisha mapato ya nchi yanaongezeka pamoja na kuboresha hali za wakulima na wadau wengine waliopo katika mnyororo wa thamani wa zao hili.

**ii. Kuongeza uzalishaji katika mafuta ya mimea kwa Kuimarisha mashamba pamoja na kukiimarisha zaidi Kiwanda cha mafuta ya Makonyo na Arki za mimea:**

Pia Wizara itahakikisha uzalishaji wa mafuta ya mimea unaongezeka kwa kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanyika za kuboresha mashamba

ya Shirika ambayo hadi kufikia sasa uzalishaji wake upo vizuri. Aidha, Wizara itahakikisha uzalishaji wa mafuta ya makonyo na arki za mimea unaongezeka kutokana na juhudi zinazoendelea za kukiboresha kiwanda.

**iii. Kampuni ya Mwani (Zanzibar Seaweed Company Ltd)**

**149. Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Baraza lako kuwa Serikali imeanzisha Kampuni ya mwani kwa madhumuni ya kuliendeleza zao hili na kutafuta masoko yenye tija. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Kampuni ya Mwani Zanzibar imeweka maeneo ya Vipaumbele kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, Vipaumbele hivyo ni pamoja na:

i. Kuimarisha ukulima wa zao la Mwani kwa kuwapatia zana za kisasa na elimu bora Wakulima wa Zao hilo pamoja na kutafuta masoko yenye tija.
ii. Kuanza ujenzi wa Kiwanda cha Mwani katika eneo lililotengwa kwa ujenzi wa kiwanda hicho huko Chamanangwe kisiwani Pemba.

**150. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, Kampuni ya Mwani Zanzibar inatarajia kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 4.7** kwa shughuli

za maendeleo ikijumuisha ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu mwani eneo la Chamanangwe kisiwani Pemba. **Shilingi milioni 444.210** zinatarajiwa kutumiwa kwa ajili ya shughuli za kawaida za Kampuni. Aidha, Kampuni inatarajia kununua Tani 1,200 za mwani wenye thamani ya shilingi bilioni 1.148 na inatarajia kupata mapato yatokanayo na mauzo ya mwani yenye thamani ya shilingi bilioni 2.031.

**151.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepangiwa matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 26.365 Kati ya fedha hizo Jumla ya shilingi bilioni 10.765 zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya kazi za kawaida na Mishahara na shilingi bilioni 15.6 kwa kazi za Maendeleo. Fedha za maendeleo ni pamoja na Shilingi bilioni 4.6 tunazotarajia kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa programu ya kuendeleza Viwanda.

**152.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ya Biashara na Viwanda imepanga kutekeleza miradi 2 ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa kuendeleza Viwanda na Mradi wa Kuimarisha Mazingira bora ya biashara iliojumuisha shughuli za kuanzisha na kuendeleza maeneo ya Viwanda, Kuimarisha eneo la Uwanja wa Maonesho wa

Kibiashara, Kutoa mikopo na kuwajengea uwezo wajasiriamali.

**153. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda itatekeleza program kuu tatu (3) na program ndogo nane (8). Programu kuu hizo kama zifuatavyo:

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara
ii. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali
iii. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

**154. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda imegawika katika Programu ndogo tatu kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Viwanda;
ii. Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara; na
iii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

**155. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ambayo inatekelezwa na

Idara ya Uendeshaji na Utumishi itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya usimamizi wa rasilimali watu na huduma za kiofisi kwa ujumla pamoja na ununuzi wa vifaa. Ili kutekeleza majukumu yake, program hii ndogo imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 1.710** kwa mwaka wa fedha 2022/ 2023.

**156.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, itakuwa na jukumu la uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda. Katika kutekeleza huduma hizo, programu ndogo ya uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti imepangiwa matumizi ya shilingi milioni 522.114 kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

**157.** **Mheshimiwa Spika,** Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo inaratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya shilingi milioni 745.368 kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

**158.** **Mheshimiwa Spika,** Ili kuweza kutekeleza shughuli zilizopangwa katika Programu kuu ya Uendeshaji

na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka 2022 – 2023, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya shilingi bilioni 2.98 kwa program hii kuu.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**159.** **Mheshimiwa Spika**, Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali imegawika katika Programu ndogo mbili kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Ukuzaji Viwanda
ii. Maendeleo ya Ujasiriamali.

**160.** **Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda, Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's na Ukuzaji wa MSME's na uendelezaji wa ujasiriamali utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na SMIDA. Ili kutekeleza huduma hii, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya shilingi bilioni 3.276 kwa mwaka 2022/2023.

**161.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ambayo ina

jukumu la kutoa kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali, Ili kutekeleza programu hii ndogo imetengewa shilingi bilioni 10.425 kwa mwaka 2022/2023.

162. **Mheshimiwa Spika**, Ili kutekeleza majukumu ya Program kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali kwa mwaka 2022/2023, naomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya shilingi bilioni 13.701 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za programu hii kuu.

## PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

163. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya tatu itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2022/2023 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo tatu (3) kama zifuatavyo:

i. Ukuzaji Masoko na Usafirishaji
ii. Uwezeshaji Biashara
iii. Utengamano wa Kibiashara

164. **Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji itakuwa na jukumu la kutoa huduma za uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara, kuongeza fursa za masoko kwa bidhaa za

Zanzibar pamoja na urahisishaji biashara ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza majukumu hayo, programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji imetengewa **shilingi bilioni 4.955** kwa mwaka 2022/2023.

**165. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara itakuwa na jukumu la kuharakisha utoaji wa bidhaa na kuboresha taratibu za utoaji mizigo pamoja na kupunguza taratibu, gharama na muda wa usafirishaji na uingizaji bidhaa nchini. Ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara, Wakala wa Vipimo, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Baraza la Taifa la Biashara, Wakala wa Usajili Biashara na Mali, Baraza la Ushindani, Taasisi ya Viwango na Baraza la Mfumo wa Utoaji Leseni. Ili kutekeleza jukumu hili, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya shilingi bilioni 4.625 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**166. Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara wenye jukumu la kuimarisha biashara huria inayopelekea upanuzi wa sokona kuongeza biashara baina ya nchi na nchi utasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza jukumu hili lililopangwa chini ya Programu hii ndogo, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **shilingi milioni 105.440.**

**167. Mheshimiwa Spika,** Ili kutekeleza huduma zilizopangwa katika Programu kuu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara kwa mwaka 2022/2023, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 9.685 kwa program hii kuu.

## 7. SHUKRANI

**168. Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Shukrani zangu pia ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, wajumbe na Makatibu wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na miongozo waliyoitoa katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara na hatimae kuridhia mapendekezo haya yawasilishwe katika Baraza hili.

**169. Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2021/2022 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa uliopatiwa Wizara yangu kutoka wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango

mkubwa wa Wadau hao kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo; Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Kimataifa la Tasnia ya Malibunifu (WIPO), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), TradeMark East Africa (TMEA), Shirika la Biashara Duniani (WTO), TANTRADE, REPOA, Zanzibar Seaweed Cluster Initiative (Zasci), Jumuiya za Wafanyabiashara, Zanzibar (ZNCC) na Wafanyabiashara na Wawekezaji wa Viwanda wote wakubwa na wadogo.

**170. Mheshimiwa Spika,** napenda nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao.

**171. Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu wa kipekee kabisa naomba kuwashukuru kwa dhati kabisa wazazi na wake zangu wote wawili kwa maombi yao ya kila siku yenye lengo la kuona napata mafanikio katika kazi zangu. Shukrani maalumu nazipeleka kwa viongozi na wanachama wa chama changu cha ACT Wazalendo ambao kwa nyakati zote wamekuwa wakinipa moyo, ushauri na hata kunikosoa pale wanapoona nakwenda kinyume na misingi ya uongozi wa umma ambayo chama chetu kinaisimamia.

**172. Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru pia kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi. Mheshimiwa Rais amekuwa mlezi kwangu na amekuwa akinionesha imani kubwa ya uongozi na ukaribu wake na miongozo yake kwangu ndio chachu ya mafanikio ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Kwa uzito unaofanana shukrani pia nazitoa kwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah.

# 8. MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## 8.1 Mapato ya Serikali

**171. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Biashara imepanga kukusanya jumla ya Shilingi 4,598,002,538 mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio vifuatavyo kama inavyoonekana katika Jadweli Namba 3:

**Jadweli Nam. 3:**

**Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022 – 2023**

| Kifungu | Maelezo | Makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 |
|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **321,860,000** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizani na Vipimo | 321,860,000 |
| | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **965,580,000** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 965,580,000 |
| | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **130,665,500** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 130,665,500 |
| | | |
| **R0106** | **Wakala wa Usajili Biashara na Mali** | **1,118,392,538** |
| 1146002 | Ada ya Utunzaji Urithi | 3,041,000 |
| 1422030 | Alama za Biashara | 483,918,000 |
| 1422031 | Uandikishaji wa Makampuni | 422,232,538 |
| 1422032 | Uandikishaji Majina ya Biashara | 125,672,000 |
| 1422034 | Ujira wa kutengeza Nyaraka | 83,529,000 |
| | | |
| **R0107** | **Taasisi ya Viwango Zanzibar** | **1,652,664,500** |

| | | |
|---|---|---|
| 1112008 | Malipo yatokanayo na Usimamizi wa Viwango | 1,652,664,500 |
| | | |
| **R0110** | **Baraza la Leseni (BLRC)** | **51,000,000** |
| 1422118 | Ada ya usimamizi wa Mamlaka za Leseni | 51,000,000 |
| | | |
| **R0104** | **Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko (DTM)** | **218,000,000** |
| 1422038 | Ada ya vibali vya usafirishaji | 218,000,000 |
| | | |
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **139,840,000** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 69,180,000 |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 35,108,000 |
| 1422034 | Ujira wa kutengeza Nyaraka | 35,552,000 |
| **Jumla Kuu** | | **4,598,002,538** |

## 8.2 Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi na ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu zake ilizojiwekea kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 26,365,400,000 kwa programu tatu (3) kama inavyoonekana katika Jadweli Namba 4:

**Jadweli Namba 4:**

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023 (TZS)**

| KIFUNGU | Programu Kuu/ Programu Ndogo | Makadirio |
|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda** | **2,977,527,000** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 1,710,045,491 |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 522,113,509 |
| SR010103 | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 745,368,000 |
| | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **13,701,922,000** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 3,276,292,000 |
| SR010202 | Maendeleo ya Ujasiriamali | 10,425,630,000 |
| | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **9,685,951,000** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 4,955,451,000 |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 4,625,060,000 |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 105,440,000 |
| **JUMLA KUU** | | **26,365,400,000** |

## 9. HITIMISHO:

173. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako na wananchi kwa ujumla kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

## 10. VIAMBATANISHO:

**Kiambatanisho Namba 1:**

### Viwanda vilivyozinduliwa na kuwekewa jiwe la msingi

| NAM | JINA LA KIWANDA | MAHALI | BIDHAA | HALI YA KIWANDA | MUELEKEO/MATEGEMEO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Zantexas Investment Co. Ltd | Amaan | Vifaa vya umeme | Uzalishaji wa nyaya za umeme (1.5mm na 2.5mm) umeanza | Bidhaa zimeanza kuuzwa katika soko la Zanzibar |
| 2. | Kiwanda cha Mafuta ya Majani ya Karafuu | Mtambwe, Mbiji, Mzambarau Baduru na Kilindi. | Mafuta ya majani makavu ya karafuu | Kiwanda kinategemea kuwa na uwezo wa kutumia kilo 2,500 za majani makavu | Kiwanda kinaendelea na upanuzi kwa maeneo mengine kisiwani Pemba |
| 3. | Quiro Group Co Ltd. | Amaan Industrial Park | Boti za uvuvi | Kimeanza uzalishaji. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha boti 7-10 zenye urefu wa mita 5-7 kwa siku | Kutengeneza boti kubwa za uvuvi zenye urefu wa mita 24 |
| 4. | YYTz | Amaan Industrial Park | Korosho | Uzalishaji umeanza | Bidhaa zake zinauzwa katika masoko ya Amerika na Ulaya (Canada, USA na UK) |
| 5. | K2 Co. Ltd | Amaan Industrial Park | Korosho | Uzalishaji wa majaribio umeanza | Bidhaa zinalengwa kuuzwa kwenye soko la Ulaya (Urusi) |
| 6. | Zanzi Quality Food | Amaan Industrial Park | Bisi (chama) | Uzalishaji umeanza | Bidhaa zake zimeanza kuuzwa soko la Tanzania Bara |
| 7. | Shear Illusion | Maruhubi | Vipodozi | Kimeanza uzalishaji | Bidhaa zake zimeanza kuuzwa Tanzania Bara na Zanzibar |
| 8. | Watercom Ltd | Kinyikani Pemba | Maji ya kunywa | Ufungaji wa mashine tayari umekamilika | Uzalishaji wa maji ya kunywa unategemewa |
| 9. | Amos Ind. Ltd | Chamanangwe | Maji ya kunywa na Juisi za matunda | Ufungaji wa mashine tayari umekamilika na kiwanda kinauwezo wa kuzalisha lita 5,000 kwa saa moja | Kuongeza laini ya juisi za matunda |
| 10. | Kassu Plastic Co. Limited | Muruhubi | Bomba za plastic | Uzalishaji wa majaribio umeanza | Upanuzi wa kiwanda unaendelea |

**Kiambatanisho Namba 2:**

## Mapato ya Wizara kwa Robo Tatu (Julai-Machi) 2021/2022

| Kifungu | Maelezo | Makadirio kwa Mwaka, 2021-22 | Makusanyo kwa Robo Tatu, 2021-22 | Asilimia ya Makusanyo kwa Robo Tatu |
|---|---|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo, Zanzibar** | **137,001,500** | **135,453,981** | **99%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 137,001,500 | 135,453,981 | 99% |
| | | | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani halali Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **583,028,000** | **620,501,000** | **106%** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 583,028,000 | 620,501,000 | 106% |
| | | | | |
| **R0105** | **Idara ya Utumishi na Uendeshaji** | **236,242,000** | **5,322,000** | **2%** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 236,242,000 | 5,322,000 | 2% |
| | | | | |
| **R0106** | **Wakala wa Usajili Biashara na Mali** | **751,394,500** | **524,004,805** | **70%** |
| 1146002 | Ada ya Utunzaji Urithi | 1,875,500 | 4,809,703 | 256% |
| 1422030 | Alama za Biashara | 360,109,000 | 183,850,355 | 51% |
| 1422031 | Uandikishaji wa Makampuni | 260,394,000 | 209,681,704 | 81% |
| 1422032 | Uandikishaji Majina ya Biashara | 77,503,000 | 71,207,044 | 92% |
| 1422034 | Ujira wa kutengeza Nyaraka | 51,513,000 | 54,455,999 | 106% |
| | | | | |
| **R0107** | **Taasisi ya Viwango Zanzibar** | **1,054,059,000** | **770,998,228** | **73%** |
| 1112008 | Malipo yatokanayo na Usimamizi wa Viwango | 1,054,059,000 | 770,998,228 | 73% |
| | | | | |
| **R0101** | **Afisi Kuu Pemba** | **73,901,000** | **88,866,366** | **120%** |
| 1422014 | Ukaguzi wa Mizania na Vipimo | 42,661,000 | 17,224,923 | 40% |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 15,483,000 | 14,487,393 | 94% |
| 1422034 | Ujira wa kutengeza Nyaraka | 15,757,000 | 57,154,050 | 363% |
| **Jumla Kuu** | | **2,835,626,000** | **2,145,146,380** | **76%** |
| | Stamp Duty (BPRA) | - | 598,810,124 | # |
| | Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko | - | 3,530,000 | # |
| | Mapato Mengineyo | - | 700,000 | # |
| **Jumla Yote** | | **2,835,626,000** | **2,748,186,504** | **97%** |

**Kiambatanisho Namba 3:**

## MATUMIZI YA PROGRAMU KWA JULAI 2021 – MACHI 2022.

| KIFUNGU | PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA | FEDHA ZILIZOPATIKANA | ASILIMIA YA KILICHOPATIKANA |
|---|---|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na uratibu wa Wizara BMV** | **3,037,903,000** | **1,821,851,941** | **60%** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 1,858,921,000 | 1,140,644,995 | **61%** |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara | 576,126,000 | 223,908,941 | **39%** |
| SR010103 | Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 602,856,000 | 457,298,005 | **76%** |
| | | | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **13,721,173,000** | **579,240,431** | **4.2%** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 3,356,988,000 | 426,085,431 | **13%** |
| SR010202 | Maendeleo ya Wajasiriamali | 10,364,185,000 | 153,155,000 | **1.5%** |
| | | | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **13,785,424,000** | **2,907,633,107** | **21%** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 4,640,773,000 | 501,572,560 | 11% |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 9,036,561,000 | 2,396,900,547 | 27% |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 108,090,000 | 9,160,000 | 8% |
| **JUMLA YA KIFUNGU RO1** | | **30,544,500,000** | **5,308,725,479** | **17%** |

## Kiambatanisho Namba 4:

### Taasisi zilizopewa vyeti vya usajili wa mikataba

- ✓ Bank Of Africa (BOA)
- ✓ BRAC Tanzania Finance LTD
- ✓ Central and Rural Development Bank (CRDB)
- ✓ Diamond Trust Bank (DTB)
- ✓ Exim Bank
- ✓ National Bank of Commerce (NBC)

**Kiambatanisho Namba 5:**

**Vikao vya kupitia viwango ambavyo ZBS imeshiriki**

i. Kikao cha Kikanda cha Afrika cha Kamati ya "Food Packaging and Labelling (ARSO TC 14);
ii. Kikao cha Kitaifa cha Kujadili Viwango vya Kikanda vya Afrika;
iii. Kikao cha Kitaifa cha Kujadili Viwango vya Kimataifa vya Codex;
iv. Kikao cha Kamati ya Kitaalamu ya Afrika (ARSO TC 03) kwa Viwango vya Samaki na Bidhaa za baharini;
v. Kikao cha Kikanda cha Afrika cha Kamati ya Maziwa na Bidhaa za Maziwa (ARSO TC 04);
vi. Kikao cha Kitaifa cha Kujadili Rasimu za Viwango vya Afrika Mashariki vya Kamati ya Samaki na Kilimo maji;
vii. Kikao cha Kitaifa cha Kujadili Rasimu za Viwango vya Afrika Mashariki vya Kamati ya Viungo;
viii. Kikao cha Kamati ya Kitaalamu ya Afrika Mashariki cha Kujadili Viwango vya Vipodozi;
ix. Kikao cha Kamati ya Kitaalamu ya TBS kwa Ajili ya Kujadili Viwango vya Afrika Mashariki vya Kemikali za Viwandani na Maabara;
x. Kikao cha Kikanda cha Afrika Mashariki cha Kujadili Viwango vya Sabuni;
xi. Kikao cha Kikanda cha Kujadili Maoni ya Nchi Wanachama ya Viwango vya Bidhaa za Nafaka vya Afrika (ARSO TC 12);
xii. Kikao cha Kitaifa cha Kamati Inayoshughulikia Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (Sanitary and Phytosanitary Measures (SPS);
xiii. Kikao cha Kikanda cha Afrika Mashariki cha Kujadili Viwango vya Vipodozi;
xiv. Kikao cha Kikanda cha NEC (National Electrotechnical Committee) Zanzibar; na,
xv. Kikao cha Kamati ya Kitaalamu ya Uhandisi Mitambo Juu ya 'Tripartite Transport and Transit Facilitation Program' (TTTFP).